Nipashe
Jumamosi Aprili 13, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581645
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**Makonda** atishia kuwataja viongozi wanaomtusi Rais UKURASA 3



**Mfamasia** atumbuliwa kisa taarifa za uongo UKURASA 4

**CHADEMA** sasa yaelekeza nguvu uchaguzi kanda UKURASA 5



**VERA SIDKA APAMBANA NA WANAOMKERA** UKURASA 12

# Vifo vya maafa ya mvua vyafikia 52

• **Nyumba** 1,035 zabomolewa, 6,874 zazingirwa maji, Mufti ataka... *Ukurasa 2*




Baadhi ya wananchi wakiangali mabaki ya gari yenye namba za usajili T 496 EFK aina ya Toyota Hiace la shule ya msingi Ghati Memorial ya jijini Arusha, wakati likitolewa kwenye Mto Mbasi, Mtaa wa Engosingiu, Kata ya Sinoni jana, baada ya kuzama katika mto huo na kusababisha vifo vya wanafunzi saba na majeruhi watatu. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Wanafunzi wanane wafariki dunia gari likizama korongoni

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akitoa heshima baada ya kuweka shada la maua kwenye kaburi la aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward Moringe Sokoine, wilayani Monduli, mkoani Arusha jana. Hayati Sokoine, alifariki tarehe 12 Aprili, 1984 kutokana na ajali ya gari iliyotokea Wami Dakawa, wilayani Mvomero mkoani Morogoro. **PICHA: IKULU**

## Rais Samia: Uthubutu wa Sokoine liwe darasa

UKURASA 3

**MICHEZO** FIFA YAIFUNGIA YANGA KUSAJILI UK.24 **MAONI,** UK.6



Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu masuala mbalimbali ikiwamo tathmini ya maafa yaliyosababishwa na mvua, miradi ya Mto Msimbazi, Bwawa la Umeme la Julius Nyerere na maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanzania yanayotarajiwa kufanyika hivi karibuni. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Vifo maafa ya mvua vyafikia 52

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema hadi sasa vifo vilivyotokana na athari ya mvua inayoendelea kunyesha na kusababisha mafuriko katika baadhi ya maeneo vimefikia 52.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, aliyasema hayo jana kupitia taarifa kuhusu mambo mbalimbali, yakiwamo maafa yaliyotokana na mvua inayoendelea.

Alisema hadi kufikia jana, kwa mujibu wa taarifa za Jeshi la Polisi, kati ya Aprili Mosi, mwaka huu hadi juzi (Aprili 11), jumla ya vifo ni 19 vilivyohusiana na mvua kubwa vimetokea katika baadhi ya mikoa.

Matinyi aliitaja mikoa hiyo ni Lindi, Njombe, Tanga, Pwani (Mkuranga na Kibaha), Manyara, Mbeya, Geita na Rukwa.

"Kimsingi nchi nzima ina hekaheka za mvua. Eneo kubwa lililokumbwa na mafuriko zaidi hadi kuhitaji Kamati ya Kitaifa ya Maafa ifanye ziara za tathmini ni mkoani Pwani katika wilaya za Rufiji na Kibiti, zilizoko kwenye ukanda wa mafuriko wa Bonde la Mto Rufiji," alisema.

Matinyi alitaja eneo la pili ni Mlimba, Kilombero mkoani Morogoro katika eneo la Bonde la Mto Kilombero.

"... Mto Kilombero huchangia asilimia 62 ya maji ya Mto Rufiji ambao hukusanya maji kutoka mikoa mingine kadhaa kwa kutumia mito ikiwamo Ruaha Mkuu na Luwegu," alisema.

Matinyi alisema mpaka sasa mkoa wa Pwani kuna vifo vitano tofauti na ripoti ya polisi ambapo Rufiji viwili na Kibiti viwili na Kisarawe kimoja na majeruhi Kibiti ni wawili na Kisarawe watatu.

Pia alisema kuna uharibifu wa mashamba ya mazao mbalimbali kama mahindi, mpunga, ndizi, ufuta, mihogo, mtama na pamba.

Kadhalika, alisema uharibifu mwingine ni wa makazi, miundombinu ya barabara, madaraja, nguzo za umeme, shule, kituo cha afya cha Muhoro kimesombwa na maji.

Alisema kata 12 kati ya 13 za wilaya ya Rufiji na kata tano kati ya 13 za wilaya ya Kibiti na moja Kisarawe zimeathirika.

"Kwa ujumla watu 126,831 wameathirika mkoani Pwani, 88,768 (Rufiji), 36,900 (Kibiti) na 1,163 (Kisarawe)," alisema huku akibainisha kuwa hekta za mashamba zilizoathirika ni 33,930.24 (Rufiji), 71,266 (Kibiti) na 167 (Kisarawe) na kwamba hadi sasa watu 1,014 wameokolewa wilayani Rufiji.

Alisema mkoani Morogoro, mvua imesababisha vifo 28 katika halmashauri nane na kubomoa nyumba 1,035 na zingine 6,874 kuzingirwa na maji. Vifo hivi ni tofauti na vya polisi.

"Ekari 34,970 za mazao mbalimbali yakijumisha mahindi, mpunga, ufuta, pamba na mazao mchanyiko zimeathirika na pia mifugo 1,466 imeathirika," alisema.

Kadhalika, alisema miundombinu ya reli, barabara, makalvati na madaraja iameharibika katika Halmashauri ya Malinyi, Mlimba, Ifakara Mji, Ulanga na Manispaa ya Morogoro imeharibika.

Alisema kamati za wilaya na za mikoa za maafa zinaendelea na kazi ya tathmini ya uharibifu na mahitaji, huku serikali ikitoa misaada mbalimbali ikiwamo inayopokewa kutoka kwa wadau.

"Tayari dawa za tiba kwa binadamu na za tiba ya maji, huduma za afya, chakula, malazi, uokoaji, usalam, ushauri nasaha, vimeanza kufikia wananchi. Askari wa wanyama pori wamepelekwa kudhibiti wanyama aina ya mamba," alisema.

Alisema jana kamati tendaji iliyoundwa na makatibu wakuu wa wizara ilikutana na baadaye itafikisha taarifa kwa Waziri Mkuu kabla ya kamati ya mawaziri kukutana haraka.

**BWAWA LA NYERERE**

Matinyi alisema licha ya kwamba kulikuwa na hatua ya lazima ya kufungulia maji ili kuuzia bwawa lisiharibike, lakini maafa ya mafuriko yamezuiwa yasiwe makubwa zaidi ya ilivyo sasa, yasitokee tangu Oktoba, mwaka jana, na kuwaarifu wananchi.

"Ingawa maji yanayopita katika Mto Rufiji yalifikia wingi wa mita za ujazo 8,445 kwa sekunde mwezi Februari, 2024 na kuendelea kwa wastani wa mita za ujazo zaidi ya 6,500 kwa sekunde, TANESCO imekuwa ikiachia kiwango cha chini zaidi ya hapo.

"Kimsingi kati ya mita za ujazo 3,000 na mara chache hadi 6,000 kwa sekunde kwa siku tofauti za mwezi Machi na Aprili, 2024, kama si kuwapo kwa bwawa hili mafuriko yangekuwa makubwa zaidi," alisema.

# Mufti na Shekhe Mkuu ataka dua maalum

**Na Romana Mallya**

MUFTI na Shekhe Mkuu wa Tanzania, Dk. Abubakar Zubeiry, amewataka mashekhe wa mikoa, wilaya, kata na maimamu kupeleka dua maalum (Kunuti) wakati wa swala ili kumwomba Mungu kuiepusha Tanzania na athari mbaya zinazotokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Mufti Zubeiry aliyasema hayo jana baada ya swala ya Ijumaa iliyoswaliwa Msikiti wa Muhammad VI, Makao Makuu ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

Aliagiza mchakato huo ufanyike kwa siku saba kuanzia jana na tayari kwa upande wa Dar es Salaam, umeanza mara moja katika msikiti huo na Mufti alewaongoza waumini walioswali hapo swala ya Ijumaa kuleta Kunuti.

Dk. Zubeiry Alisema Kunuti ambayo iliswalishwa na Sheikh Muhammad Nassoro ambaye ni Mkuu wa Itifaki Bakwata Makao Makuu na Rais wa Qur'ani nchini Tanzania.

# Wanafunzi wanane wafariki dunia gari likizama korongoni

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WANAFUNZI wanane wa Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya Ghati Memorial ya jijini Arusha, wamepoteza maisha baada ya gari dogo aina ya Toyota Hiace yenye namba za usajili T 496 EFK kuzama kwenye korongo lenye maji mengi yanayotokana na mafuriko ya mvua za masika zinazoendelea kunyesha.

Miili sita iliopolewa jana jioni wakati mwili wa mwanafunzi mmoja uliopolewa jana muda mfupi baada ya kuzama.

Wakati wanafunzi hao wamefariki dunia, wengine watatu pamoja na mwalimu wao, wamenusurika kifo baada ya kuokolewa na wananchi na kupelekwa katika Kituo cha Afya Muriet kwa matibabu.

Glory Daniel (8) mmoja wa manusura wa ajali hiyo, anayesoma darasa la pili, alisema gari hilo lililokuwa linaendeshwa na Lukuman Hemed, walipofika eneo la tukio majira ya saa 12:00 asubuhi, dereva huyo aliambiwa na mwalimu asivuke hapo kwa kuwa maji ni mengi, lakini alimwangalia mwalimu huyo na kuanza kucheka kisha akataka kuvuka.

Gloria ambaye ni ndugu na Praygod Daniel (10) na mwenzao Rose Immanuel (10) anayesoma darasa la tano na mwalimu wao Anastazia Immanuel (27), wamelazwa kituoni hapo na hali zao zinaendelea vizuri.

Ajali hiyo ilitokea katika korongo lililoko eneo la Engosheratoni, kata ya Sononi baada ya kuvutwa na maji hayo yaliyokuwa yamevuka kimo cha daraja.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, alithibitisha kuwa basi hilo lilikuwa na watu 13, kati yao 11 wakiwa wanafunzi wa shule hiyo. "Hali si shwari kama mlivyosikia na kama ulivyojionea. Gari la Ghati Memorial School limetumbukia kwenye mto (korongo). Ilikuwa ni majira ya saa 12:00 asubuhi.

"Mnafahamu kabisa kwamba mvua zilikuwa ni nyingi sana kuanzia usiku mpaka alfajiri mvua zilikuwa zinanyesha. Lakini wakati dereva anapita watu walimuambia kwamba haya maji huwezi kukatiza.

"Dereva aliendelea kukaidi akalazimisha, baada ya kulazimisha alivyoingiza gari tu likavutwa likaingia mtoni. Gari lilikuwa na jumla ya watu 13, wanafunzi walikuwa 11, dereva mmoja na matroni mmoja ambaye ni mwalimu. Waliookolewa jumla yao ni watano, wanafunzi wakiwa watatu, dereva mmoja na mwalimu mmoja," alisema.

Kwa mujibu wa Mtahengerwa, hadi jana mchana, waokoaji walikuwa wameuopoa majini mwili wa mwanafunzi mmoja ambaye kwa bahati mbaya walikuta amepoteza maisha.

Kuhusu uokoaji, Mkuu huyo wa Wilaya alisema: "Kwa hiyo kazi inayofanyika sasa hivi ni kuendelea kuhamasisha wananchi kuambaambaa na huu mto ili tuweze kujua wenzetu saba ambao hatuwaoni wako wapi. Kwa wale ambao hatujawapata wako wapi, tuendelee kuwa wavumilivu."

Mbunge wa Arusha (CCM), Mrisho Gambo, akizungumzia tukio hilo, alisema changamoto ya eneo hilo ni ya muda mrefu na wanaostahili kutupiwa lawama kutokana na ajali hiyo ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wanaozuia kujengwa kwa daraja eneo la Sinoni ilipotokea ajali.

"Changamoto iliyokuwepo wenzetu wa TANESCO wamekuwa wanakataa daraja lisijengwe. Hata ukienda kule kwenye kata ya Lemara pia tumepata mpaka fedha za kujenga daraja lakini TANESCO wanakataa. Cha kushangaza hata kama daraja hakuna wananchi wanapita, magari yanapita.

"Sasa tumepata madhara makubwa kama haya, ni vizuri wenzetu waone watoto saba hawaonekani, mmoja ameokolewa amekufa na wengine wamekuwa majeruhi.

"Hatuwezi kuzuia kitu kwa sababu tu ya sababu zao, wakati maisha ya watu yanapotea. Kwa hiyo mimi ombi langu kwa serikali, kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda na Ofisi ya Waziri Mkuu, ambao wanashughulika na maafa nchini.

"Tuhakikishe kwamba wenzetu wa TANESCO wanatumia busara na hekima ili watoe fursa kwa wenzetu wa TARURA (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini) wajenge daraja hapa na tuokoe maisha ya watoto wetu; maana hili jambo ni jambo kubwa, ni jambo gumu na ni masikitiko makubwa sana katika Jiji letu, lakini lakini pia katika Jimbo letu la Arusha," alisema. Hapa kwenyewe (Sinoni) tunajenga hoja kila siku. Wenyeviti wa serikali za mitaa wamejenga hoja, diwani wa kata hii amejenga hoja na wananchi imekuwa ni kilio chao cha siku nyingi lakini watu wa TANESCO wamekuwa ni kikwazo," aliongeza.

Mmoja wa mashuhuda wa ajali hiyo, Fedrick Kikukwa, alisema wanaiomba serikali kuwasaidia kujenga daraja katika barabara hiyo ya Sinoni/Lemara na si kivuko kwa sababu maafa yanayojitokeza yatakuwa makubwa zaidi.



Wakazi wa Kijiji cha Barikiwa, Kata ya Barikiwa wilayani Liwale mkoa wa Lindi, wakichota maji kwenye chemchemi, kijijini hapo, kwa ajili ya matumizi ya nyumbani baada ya bomba la maji la kijiji kuharibika na kusababisha uhaba wa bidhaa hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia: Uthubutu wa Sokoine liwe darasa

**Na Allan Isaack,** MONDULI

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameagiza viongozi wote wa serikali wakiwamo wanaotokana na mamlaka yake ya uteuzi, kusimamia maagizo wanayopewa bila kutetereka na kuiga uthubutu wa Waziri Mkuu wa zamani, Hayati Edward Moringe Sokoine.

Akizungumza jana katika kumbukizi ya miaka 40 ya Sokoine iliyofanyika nyumbani kwa Hayati Sokoine, Monduli Juu mkoani Arusha, alisema ni lazima viongozi wa umma watekeleze maagizo yake bila kuyumbishwa.

"Somo tunalolipata kutoka kwa Marehemu Sokoine, ni kuwajibika kwa kuwa alisimama kutokana na mienendo na matendo yake kama kiongozi.

"Hapa nataka kusisitiza kwa viongozi kusimamia maamuzi ya serikali. Kwamba uamuzi ukifanyika kifuatacho, ni utekelezaji tu na viongozi wa serikali ni lazima watekeleze uamuzi kama ilivyoafikiwa bila kuyumbishwa na ikiwezekana wawe mfano kwa wengine," alisema.

.Rais Samia alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, kuweka utaratibu wa kuhifadhi kumbukumbu muhimu za viongozi wa kitaifa nchini.

Kwa mujibu wa Rais Samia, Sokoine alikuwa mpenda maendeleo kwa kuwa kwa nyakati tofauti, alisisitiza kazi kubwa kwa wanazuoni ni kuongeza mijadala kuhusu namna nchi inavyoweza kujiletea maendeleo.

Pia alisema Sokoine aliwataka kuhakikisha mawazo yao namna ambavyo yanaweza kuwaletea maendeleo wananchi kwa watunga sera, vyama vya siasa na watendaji wa serikali.

"Naikumbuka kauli yake kuhusu elimu inayotakiwa kwa ajili ya maendeleo vijijini ni kuimarisha na kuinua ustaarabu ili watu wasiridhike na maisha duni waliyo nayo na elimu ya aina ya pili, ni ufundi na tatu, ni ile ya kuelewa mazingira ya kijamii, ili watu waelewe nafasi yao katika jamii wanayoishi,"alikumbusha Rais Samia.

Alisema serikali imefanyia kazi kwa kiasi mawazo hayo kwa kuwa kuanzia Februari, mwaka huu, imeanza kutekeleza sera ya elimu iliyoboreshwa inayojielekeza kuleta mageuzi makubwa vijijini.

Miongoni mwa maboresho yaliyofanyika, alisema ni kuweka msisitizo kwenye elimu ya ujuzi ili wanafunzi wakihitimu wawe na uwezo zaidi wa kuchangia katika jamii na kutumia fursa zilizoko.

"Ili tuweze kukuza uchumi wa nchi yetu na kuleta mageuzi vijijini, ni lazima tuwe na vijana wenye elimu ya ufundi na mafunzo ya stadi za kazi na kwa kuzingatia dhana ya maendeleo ya mageuzi vijijini, serikali imeendelea kuboresha huduma za jamii na miundombinu nchini kwa kasi.

"Mfano kwa hapa Monduli kuanzia mwaka 2021 tumejenga Shule ya Msingi Emairete, tumejenga Shule za Sekondari Meserani, Mswakini na Lepurko ambayo imefunguliwa hivi Karibuni.

"Wanafunzi 40 tayari wameshaingia. Shule ya Sekondari ya Lepurko iko vizuri na imejengwa kwa mfumo wa ghorofa ila wanafunzi waliopo ni 40, hivyo naomba ndugu zangu wa kimasai pelekeni watoto kwenye ile shule ili ikatumike kikamilifu," alisisitiza.

Alisema ili kuhakikisha lishe bora kwa wanafunzi, serikali inatumia Sh.bilioni saba kwa ajili ya chakula kwenye shule za Wilaya ya Monduli kama njia ya kuenzi mawazo ya Sokoine.

Rais alisema kwa kuwa Sokoine alitoa eneo lake kwa Kanisa Katoliki kwa ajili ya kujenga Chuo cha Ufundi kusaidia kuleta mageuzi, lakini hadi sasa bado hakijajengwa.

"Natoa rai kwa kanisa kwa kushirikiana na viongozi wa serikali kutimiza azma ya Sokoine na kama kuna mkwamo naomba tuwasiliane kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha ili tukwamue na chuo kijengwe," aliagiza.

Kuhusu sekta ya afya, Rais Samia alisema tayari kuna kituo cha afya kimejengwa na serikali katika kijiji cha Nafko, Kata ya Loksale. Pia serikali ina mpango wa kufanya ukarabati kwenye hospitali kongwe za wilaya, utakaohusisha majengo, vifaa tiba na kupeleka wataalamu wa afya.

Pia aliahidi katika mpango wa bajeti, mwaka ujao serikali imepanga kujenga barabara kutoka kijiji cha Ngarash mpaka Monduli Juu ambako kuna makazi ya Waziri Mkuu wa zamani, Hayati Edward Ngoyai Lowassa na Hayati Sokoine.

Kuhusu maji, alisema kuna mradi wa maji wa Sh. bilioni 20 utakaopeleka maji kutoka jijini Arusha na kusambaza kwenye vijiji 13 vya Monduli. Pia alisema uko mradi mwingine unaotekelezwa na serikali ukihusisha vijiji vya Makuyuni, Naiti, Mbuyuni na Lesimiongori wenye thamani ya Sh. bilioni saba.

**MTOTO AMWAGA CHOZI**

Kiongozi wa Familia ya Hayati Sokoine, Balozi Joseph Sokoine, alibubujikwa na machozi wakati anasoma wasifu wa baba yake,.

Alisema Sokoine alikuwa anapenda kufanya kazi kwa bidii bila kuchoka, alikagua na kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo, alitenga muda wake wa kuwa na familia hasa alipokuwa likizo na alipenda kutunza mazingira kwa ajili ya mifugo yao.

Pia alisema alikuwa kinara wa kutunza mazingira kwa kupanda miti maeneo mbalimbali katika jamii na alikuwa mstari wa mbele kuhimiza jamii kupanda miti. Alisema alitambua mchango wa elimu kwa usawa kwa watoto wa kike na wa kike kwa jamii ya kifugaji ya maasai .

Alisema kwa kuwa jamii ya Monduli ni jamii ya kifugaji Sokoine alifanikisha ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhia maji kwa ajili ya kunywesha mifugo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema utaratibu wa kutunza viongozi, unaleta umoja na msimamo kwa kuwa unatoa fursa kwa watu kuendeleza kuyaenzi mambo yote mazuri wakati walitumikia taifa kipindi cha uongozi wao.

## Makonda atishia kuwataja viongozi wanaomtusi Rais

**Na Beatrice Shayo,** MONDULI

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda amesema anawajua kwa majina yao na atawataja hadharani mawaziri ambao ni wateule wa Rais Samia Suluhu Hassan wanaomtukana.

Kutokana na kudai kuwapo kwa watu hao Makonda ametangaza kiama chao, akisema atawataja mawaziri hao ifikapo Jumatatu ijayo endapo wataendelea na tabia hiyo.

Akiwa katika kumbukizi ya miaka 40 ya Waziri Mkuu wa zamani, Hayati Edward Moringe Sokoine, Monduli Juu mkoani Arusha, Makonda alisema anataka iwe mwisho kwa wateule hao kuwatuma watu wanaomtukana Rais Samia kwenye mitandao ya kijamii.

"Hasa kaka zangu mnaotuma watu kumchokoza mama yangu Rais Samia, mnajijua na mimi ninawajua. Mheshimiwa Rais, kwa majina yao nawajua na leo Aprili 12, mwaka huu, nataka iwe mwisho kuwatuma watu wale wanaokutukana kwenye mitandao ya kijamii.

"Jumatatu (Aprili 15), wakiendelea nitawataja majina yao na wengine ni mawaziri na wengine wanapewa nguvu na watu tuliowaheshimu. Naomba iwe mwisho, tumuache Rais Samia afanye kazi yake," alisema.

Kuhusu athari za mafuriko kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, Makonda alisema Aprili 8 hadi 12, mwaka huu, kumekuwa na mvua ambayo haijawaacha salama wakazi wa mkoa wa Arusha kwa kuwa wameathiriwa na miundombinu na wananchi nyumba zao zimejaa maji na tope huku wengine wakikosa makazi.

Makonda alisema wamepoteza ndugu zao sita kutokana na mvua inayoendelea kunyesha na kuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. "Rai yangu madereva wanaoendesha vyombo vya moto wawe makini. Leo (jana) asubuhi, nimepewa taarifa ya dereva aliyekuwa amebeba wanafunzi wa shule, wenye umri kuanzia miaka mitano hadi 12, aliyelazimisha kulipitisha basi na kusababisha kifo cha mwanafunzi mmoja na wengine saba mpaka sasa tunaendelea kuwatafuta.

"Nitoe rai kwa madereva wa magari, bodaboda na wengine wanaoendesha vyombo vya moto. Pale wanapoona mvua inanyesha na yapo maji mengi ni vyema wakawa na subira tusije kuingiza taifa na falimia katika majonzi makubwa," alisema.

Aidha, Makonda alimshukuru Rais Samia kwa kazi kubwa anayoifanya, akieleza tayari ameiona Sh. trilioni 1.8 zimeshafika katika mkoa wa Arusha katika kumuenzi Hayati Sokoine.

Alisema serikali imeamua kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, kilometa 11.66 kutoka Ngarashi hadi Monduli Juu.

Kwa mujibu wa Makonda, upendo wa Rais Samia hivi sasa unaendelea kutokana na kuijenga barabara kuu ya Arusha -Moshi inayokwenda Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

"Nia ya kuijenga barabara ya KIA, ni ili watalii wanapokuja katika Mkoa wa Arusha, wasipate mateso. Serikali itaanza kwa kujenga kilometa 25 na kadri ya uwezo fedha kupatikana, tutaongeza na hatimaye kufika KIA. Nakushukuru kwa barabara ya Kisongo kwenda kwenye Soko la Kilombelo, barabara hiyo itasaidia kuongeza chachu ya maendeleo.

Mheshimiwa Rais, nina ombi langu la mwisho. Moja ni kazi uliyonipa ya utalii. Mji wetu ni mji wa kitalii, tumeshakaa vikao vingi tumekubaliana jiji la Arusha kufungwa kamera na kuhakikisha taa zinawaka. Kutakuwa na polisi wa kitalii, watapita na baiskeli kuimarisha ulinzi.Tunataka ifike hatua hata mtalii anatamani kupiga picha na Polisi hao wanaoimarisha ulinzi," alisema.

Makonda alisema amemeagiza kuondolewa kwa mabango yote yanayochafua Jiji la Arusha, na kuhakikisha panakuwa na muonekano mzuri ili watalii watakapofika wasiwaone ni watu ambao hawawezi kuwa na mazingira bora.

# Mfamasia halmashauri atumbuliwa jokofu nyumbani kuhifadhia damu

**Na Vitus Audax**

MKURUGENZI wa Huduma za Afya Ustawi wa Jamii na Lishe Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Rashid Mfaume, ameagiza Mfamasia wa Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga kuondolewa kwenye nafasi hiyo kwa kutoa taarifa ya uongo.

Mfamasia huyo anadaiwa kutoa taarifa kinzani na uhalisia wakati wa ukaguzi wa vifaa katika kituo cha afya Mwalugulu, hivyo kusababisha kupokewa kwa vifaa tofauti na vilivyoagizwa. Dk. Mfaume alifikia uhamuzi huo juzi baada ya kubaini ukiukwaji wa ununuzi wa vifaa yakiwamo majokofu ya kuhifadhia damu kituoni hapo wakati akikagua shughuli za uendeshaji na usimamizi wa shughuli katika kituo cha afya.

Katika ukaguzi huo, Dk. Mfaume alieleza kubaini majokofu mawili ya matumizi ya nyumbani yaliyonunuliwa katika kituo hicho kwa gharama za majokofu ya kuhifadhia damu kinyume cha taratibu za ununuzi pamoja na sheria na taratibu kiafya.

"Walipokea vifaa hivi vikiwa vimefungwa na hawakufanya ukaguzi wa aina yoyote na leo (juzi) tumekuta vimefungwa lakini mfamansia anatudanganya kuwa walivikagua. Pia majokofu haya kwa ndani yameelekeza matumizi yake kuwa ni ya matunda aina ya nyanya, karoti na parachichi na matunda mengine na si damu," alisema.

Pia alisema tayari wataalamu wamethibitishia kuwa hayo si majokofu ya damu na gharama zake hazizidi Sh. milioni 1.5 lakini yamenunuliwa kwa Sh. milioni 3.8 na yamepokewa na mzabuni akalipwa fedha bila kufanyika ukaguzi.

Dk.Mfaume pia alimwagiza elekeza mganga mkuu wa mkoa huo kuiandikia barua ya onyo timu ya usimamizi wa shughuli za afya ya halmashauri (CHMT) ya Msalala ikiongozwa na Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo kutokana na uzembe katika usimamizi na ufuatiliaji uliobainika.

Pia Dk. Mfaume baada ya kubaini kuwapo kwa usimamizi mdogo katika ununuzi, aliielekeza timu ya usimamizi shughuli za afya mkoa (RHMT) kufuatilia wote ambao wamenunua vifaa na vifaatiba mkoani humo na kubaini uhalali wa vifaa hivyo.

"Tukiondoka tu waingie kazini kufuatilia ushirikishwaji wa watumishi na wataalamu wakati wa kuanza na kupokelewa kwa vifaa hivyo pamoja na uwapo wa barua za kuundwa kwa kamati za mapokezi ya bidhaa pamoja na taarifa zake.

Pia alielekeza kupewa barua za onyo kwa timu ya huduma za afya ya halmashauri hiyo kwa kutoa taarifa kubaini kutokuwapo kwa makusanyo ya fedha katika hospitali hiyo tangu mwaka 2022 ilipoanza kufanya kazi.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akisalimiana na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda alipowasili mkoani humo juzi, kwa ajili ya kushiriki Ibada Maalum ya kumbukizi ya Miaka 40 ya kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward Moringe Sokoine. **PICHA: OMR**

## Mvua yasababisha uharibifu wa mali, ukosefu wa makazi

**Na Vitus Audax**

ZAIDI ya nyumba 50 katika Mtaa wa Mbugani, Halmashauri ya Geita, mkoani hapa, zimeharibiwa na mvua inayoendelea kunyesha hali iliyosababisha wananchi kukosa makazi na kulazimika kuomba hifadhi kwa ndugu wa maeneo jirani.

Mvua hiyo ambayo chanzo chake kinadaiwa ni kuziba kwa mitaro baada ya mchanga kujaa na hivyo kusababisha maji kwenda katika makazi ya watu, zimesomba pia mazao pamoja na mifugo.

Mkazi wa Mtaa huo, Velanus Dominick, alisema maji yamesomba vitu vya ndani yakiwamo magodoro na baadhi vimekutwa mtaa Lake View jirani na kulikotokea tatizo hilo.

"Kuna bibi tumemwokoa alikuwa anakwenda na maji. Maji yalikuwa na kasi kubwa yamesomba mifugo kama bata, kuku na Mbuzi,"alisema.

Dominick alisema mitaro hiyo imekuwa ikijaa maji mara kwa mara na kwenda kuathiri makazi na wamekuwa wakiomba mamlaka husika zifanye marekebisho ili kunusuru na adha hizo.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Geita, Mhandisi Bahati Simbeye, alithibitisha kutambua kero hiyo ambayo imesababishwa na wananchi kuendesha shughuli za kilimo karibu na daraja lililoko eneo hilo.

"Ninachoweza kukwambia ni kuwa, huo mtaro unatoa maji kwenye mitaa mbalimbali ya Mji wa Geita na kuziba kwake kunasababishwa na wananchi wenyewe wanaofanya shughuli za kilimo karibu na eneo hilo," alisema Mhandisi Simbeye.

Alisema wananchi wanaoendesha shughuli za kilimo maeneo hayo wamekuwa wakiuchimba, hivyo kusababisha maji kuacha njia yake na kwenda katika makazi.

"TARURA tumekuwa tukienda kutoa mchanga na kuzibua unapoziba, kwa hiyo tatizo ni wananchi wenyewe. Tunatumia nguvu nyingi kuwaelimisha kuhusu madhara ya namna hii, lakini wanaona tunawazibia riziki. Madhara yake ndio hayo, maji yanavamia makazi yao," Mhandisi Simbeye.

# Mradi Bonde Msimbazi kuanza rasmi Jumatatu

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema Mradi wa Bonde la Msimbazi, Dar es Salaam unatarajia kuanza rasmi keshokutwa (Jumatatu), ukisimamiwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini Tanzania (TARURA).

Mratibu wa Miradi ya Ushirikiano na Benki ya Dunia na TARURA, Humphrey Kanyenye, katika taarifa yake ya awali, alisema ubomoaji wa nyumba ili kupisha mradi huo ungeanza jana.

Jana, Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, katika taarifa yake kuhusu mambo mbalimbali ukiwamo mradi huo, akisema unatarajia kuanza Aprili 15, mwaka huu.

Alisema mradi huo utaanza kwa kubomoa nyumba katika maeneo ya Jangwani, kandokando ya Mto Msimbazi.

"TARURA itaanza mradi huu kwa ubomoaji kwa kuzingatia makubaliano yake na wakazi wa eneo hili kwamba nyumba zao zitafanyiwa tathmini, watalipwa fidia na wiki sita baada ya fedha kuingizwa kwenye akaunti zao, TARURA itavunja nyumba katika eneo husika," alisema.

Matinyi alisema hadi kufikia Februari 29, mwaka huu, TARURA imeshaingiza malipo ya fidia ya jumla ya Sh. bilioni 52.61 katika akaunti za wamiliki wa nyumba 2,155 kati ya 2,329 walioandikishwa katika daftari la kwanza.

"Hivi sasa TARURA inakamilisha malipo ya fidia kwa wahusika wengine 446 waliomo kwenye daftari la pili ambao hawakufanyiwa uthamini wa awali kwa sababu mbalimbali," alisema.

Pia alisema TARURA itashirikiana na ofisi za halmashauri za mkoa wa Dar es Salaam katika maeneo ambayo mradi unapita ili kuhakikisha kazi inafanyika kwa usahihi na umakini.

Alisema TARURA inawashauri wananchi watakaokuwa na maswali kuhusu mchakato huo kupiga simu namna 0738 353854 au 0738 353855 iwapo watahitaji ufafanuzi wowote.

**MIAKA 60 MUUNGANO**

Matinyi alisema maadhimisho ya sherehe za kitaifa za miaka 60 ya Muungano zinatarajia kufanyika katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na mgeni rasmi atakuwa Rais Samia Suluhu Hassan. Alisema uzinduzi wa sherehe hizo utafanyika kesho katika Uwanja wa Michezo wa Amani, Zanzibar, ambako mgeni rasmi atakuwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

"Aprili 25, mwaka huu, kutakuwa na tamasha la miaka 60 ya Muungano litakalofanyika katika wilaya zote lakini kwa Dar es Salaam litafanyika katika viwanja vya Tanganyika Packers, Kawe na mgeni rasmi atakuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko.

Aprili 8, mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alizindua kaulimbiu na nembo ya maadhimisho hayo isemayo "Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Tumeshikamana na Tumeimarika kwa Maendeleo ya Taifa Letu."

Nembo iliyozinduliwa inatakiwa kutumika katika nyaraka za serikali, matangazo, mialiko, mapambo na pia kutumika kwenye vituo vya televisheni vya umma na binafsi katika kipindi cha kusherehekea miaka 60 ya Muungano.

# CHADEMA yaelekeza nguvu uchaguzi kanda

**Na Vitus Audax**

BAADA ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kukamilisha uchaguzi wa ndani ngazi za mikoa na wilaya, sasa kimetangaza kuanza uchaguzi wa viongozi ngazi ya kanda kuanzia Mei, mwaka huu.

Uchaguzi wa viongozi wa kanda unatarajiwa kufanyika katika Kanda nne za kiutawala katika chama ambazo ni Victoria yenye mikoa ya Mwanza, Kagera na Geita, Serengeti(Mara, Shinyanga na Simiyu), Magharibi(Tabora, Kigoma na Katavi) na Nyasa (Iringa, Mbeya, Njombe,Songwe na Rukwa).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA (Bara), Benson Kigaila, hatua hiyo ni kwa mujibu wa Kanuni za CHADEMA, Kanuni ya 7.3.1.

Alitaja nafasi zinazogombewa kuwa ni Mwenyekiti wa Kanda, Makamu Mwenyekiti, Mweka Hazina wa kanda, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina wa Kanda wa Baraza la Wazee Chadema (BAZECHA).

Nafasi nyingine ni Baraza la Wanawake (BAWACHA) ambazo ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina huku Baraza la Vijana (BAVICHA) zikigombewa nafasi ya Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina. Kigaila alisema fomu za kugombea nafasi hizo zinapatikana katika ofisi za kanda husika, makatibu wa mikoa na kwenye tovuti ya chama kuanzia jana na mwisho wa kurejesha ni Aprili 22, mwaka huu, saa 10:00 jioni.

Pia aliwataka watia nia kuambatanisha fomu zao wakati wa kuzirejesha pamoja na risiti ya malipo fomu ambayo ni Sh.100,000 inayotakiwa kulipwa kwenye akaunti ya benki ya kanda husika.

Uchaguzi wa viongozi wa chama hicho ngazi ya mikoa na wilaya katika baadhi ya kanda ulitamatika mwishoni mwa mwezi uliopita, hivyo kutoa fursa kwa sura mpya kushika nyadhifa mbalimbali.



Baadhi ya Watumishi wa Chuo cha Sayansi za Afya Kolandoto na Manispaa ya Shinyanga, wakiwa katika Kivutio cha Utalii katika Chemchem ya Maji Moto jana, ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha utalii kwa kuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa akihamasisha masuala ya Utalii. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Askofu akemea jamii kukubali utumwa

**Na Isack Allan,** MONDULI

Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha, Isaac Amani, amekemea tabia ya baadhi ya watu kukubali utumwa na umaskini kiama ndio mfumo wa maisha.

Askofu Mkuu Amani alisema hayo jana wakati wa hafla ya kumbukizi ya miaka 40 ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, Hayati Edward Sokoine iliyofanyika Monduli Juu, wilayani hapa.

"Hatuwezi kukubali hali ya utumwa kuwa ni ya kawaida kwa kuwa kristo ametufundisha tusikubali hali ya utumwa kuwa ni ya kawaida kwa kuwa hatuwezi kuwa tumeumbwa kwa mfano wake wakati tuna dhambi.

"Hatuwezi kutawala viumbe vingine wakati tumefungwa kwa dhambi ikiwamo ulafi kwa kuwa unakula tu mpaka unavimbiwa na uzembe hasa pale unapotumainiwa kufanya jambo lakini haufanyi kwa kuwa unaleta hasara kwa jamii

"Pia wivu ukitokota ndani mwako unajikuta unahangaika kuwashusha wale ambao wamepanda juu kwa kuwa unafurahia unapodidimiza wenzako. "Kadhalika uvivu unajikuta umekaa kiuvivu uvivu tu na maisha yako yanakuwa ni ya kuteleza na sio ya kuzalisha.

"Ufisadi na ubinafsi unaweza kukupeleka mahali ambapo unakandamiza maslai ya wengine kwa ajili yako mwenyewe, sambamba na ubaguzi ambao uchangia kukosekana kwa misingi ya kukosekana kwa haki na hasira kwa kuwa familia nyingi zimeumia kutokana na hasira yako.

"Chuki na mambo hayaendi japokuwa yako kwenye mpangilio chuki ikiwepo hayawezi kwenda,pamoja na majivuno kwa kujifunia hakuna mtu yeyote ambaye atakufanya kitu chochote," alisema.

Alisema Yesu Kristo aliweka wazi kuwa kwa kuwa wakati wa Ufalme wa Mungu umetimia watu watubu na kuiamini injili na kufanya toba ya kujirekebisha,namna ya kufikiri na kutenda,kutathimini wazoea na kujenga kweli namna ya kwenda vizuri na matendo ya Mungu.

"Mwaga takataka kwenye glasi yako ili uongezewe kinywaji safi na kukaribisha mambo mazuri kwenye ufalme wa Mungu kwa unawafungua watu macho kuwa na akili ili watembee katika mwanga wa ukweli na haki pasipo kuwakanyaga wengine,msimalizane bali tuimarishane," alisema.

Pia aliwataka Watanzania kuwa wakarimu hawa kwa walionacho kwa wale wasionacho na kulipa kodi na Serikali inapaswa kuwahudumia wananchi kupitia kodi ili kuleta maendeleo kwa nchi.

"Wahitaji watakuwapo kwa kuwa jamii inawatengeneza kila wakati kwa kuwa kuna wavivu ambao wanakula na wanastahili kutunzwa, kuna wagonjwa ambao hawajiwezi,wako waliopatwa na mahafa kwa kuwa haukuwa mpango wao kupata shida hizo,vita,moto ukitokea na kuteketeza mali zao hivyo usidharau mchango wako wa kuwasaidi wenye dhiki," alisema.

Alisema Hayati Sokoine alikuwa kiongozi hodari na mkweli na alijutoleza kama mche wenye nguvu na taifa lilipata kijana mdogo ambaye alikuwa anajua mambo mengi hasa kuangalia nchi ilikuwa inakwenda wapi aliangaika kufanya hivyo.

"Alikuwa kiongozi hodari mwenye uzalendo na tulipata fahari kumwona kama shujaa wetu ambaye alikuwa mkereketwa wa maendeleo kwa kuwa maneno yake yalileta faraja na matumaini wananchi kutokana na ukweli wake na alipiga vita uhujumu uchumi na waliomfahamu walimtambua kwa hiko.

"Mambo ya ufisadi na leo angekuwa hai angetuambia tujihadhari na jani la Arusha (bangi),kwa kuwa vijana wanaangamia katika jani hilo na wanaouza madawa hayo wanatakiwa kutafutwa na kushughulikiwa kisheria ili tuweze kuwa na maendeleo ya kweli na watu wenye akili na sio mazezeta.

"Sokoine alikuwa chachu ya kusaidia jamii ya watu Maasai kutokea suala la kupeleka shule, kwa kuwa alitambua kabila hilo wanavipaumbele vyao lakini sio shule hivyo alihamasisha angalau kila familia moja kupeleka watoto shule.

# CCM yajigamba ushindi ni lazima

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetangaza kinatarajia kuanza ziara katika mikoa sita kuanzia leo huku kikijigamba kuwa ushindi katika uchaguzi ujao ni lazima.

Ziara hiyo itahusisha viongozi wa chama hicho ambao ni Katiba Mkuu, Dk. Emmanuel Nchimbi na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dodoma wakati wa hafla ya mapokezi ya wajumbe wa Sekretarieti ya Chama hicho Taifa katika Ofisi za CCM Makao Makuu.

Naibu Katibu Mkuu CCM Bara, John Mongella, alisema ili kufanikisha ziara hiyo tayari ametoa magari 10 yenye vipaza sauti, mafuta na posho za kujikimu kwa timu nzima itakayokuwa katika msafara huo kwenye mikoa sita ya awali na baadaye nchi nzima.

Mongella alisema kupitia timu yao aliyoiteua hivi karibu Rais Samia Suluhu Hassan, wanatarajia ifikapo Oktoba, mwaka huu, watakuwa wamepata idadi kamili ya kura watakazozipata katika uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na madiwani utakaofanyika mwakani.

"Ndiyo maana baada ya sisi kuteuliwa, wote tulipimwa afya maana Rais (Samia Suluhu Hassan) hataki mtu mgonjwa na wote tuligundulika kuwa tuko sawa, hivyo tutahakikisha timu yetu hii inaleta ushindi ndani ya chama katika uchaguzi mkuu na wa serikali za mitaa, hata kama VAR itagoma ushindi kwa CCM ni lazima," alisema.

Mongella alizitaka kamati za siasa kuacha kufanya mikutano ya ndani badala yake iitishe mikutano ya hadhara ya wananchi na kuzungumza nao mambo yaliyotekelezwa na serikali ya awamu ya sita.

Naye Makalla alisema yuko tayari kushiriki mdahalo wowote utakaoandaliwa kwa ajili ya kukitetea chama kwa hoja na siyo vioja.

Alisema CCM ina imani kubwa ya kushinda katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kutokana na kazi kubwa ambayo imefanywa na serikali.

"Kesho (leo) tunanza ziara ya mikoa sita. Lengo ni kwenda kuanza maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani. tutakutana na wananchi na kuwaeleza umuhimu wa kushiriki kupiga kura, lakini pia kusikiliza na kutatua kero za wananchi pamoja na kukagua utekelezaji wa Ilani ya chama," alisema.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Malengo mashindano ya CAF msimu ujao yaende na uhalisia

**BAADA** ya timu zake kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwenye misimu minne iliyopita, Tanzania sasa inauhakika wa kuingiza klabu nne katika michuano inayosimamiwa na shirikisho hilo.

Kila mwaka CAF huandaa na kusimamia mashindano yake ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na michuano ya Kombe la Shirikisho.

Msimu huu unaoendelea na uliopita, Tanzania iliwakilishwa na timu nne, mbili zikishiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na nyingine zilipeperusha bendera yake kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho.

Simba na Yanga zote za Dar es Salaam zenyewe zilikuwa zinashiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati katika mashindano ya Kombe la Shirikisho, Azam FC na Singida zilipeperusha bendera ya Tanzania Bara.

Lakini pia kwa upande wa Zanzibar, KMKMK na JKU pia walishiriki mashindano hayo ya kimataifa.

Msimu wa mwaka jana tulishuhudia kwa mara ya kwanza, Yanga ikitinga hatua ya fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho (ilifungwa na Waarabu wa Algeria- USM Alger), huku Simba ikiishia hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Msimu huu, vigogo hao wa Tanzania wote wameishia hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga ikiondolewa na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini na Al Ahly ya Misri ikizima tena ndoto za Simba kusonga mbele kwa kuwafunga kwenye mechi zote mbili walizocheza za hatua hiyo.

Ili kufanya vizuri katika mashindano ya ndani au ya kimataifa, timu husika inahitaji uwekezaji wa kweli. Uwekezaji wa kweli ndio husaidia kufikia malengo na si vinginevyo.

Kama timu yako malengo yake ni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara au michuano ya Kombe la FA, ni lazima usajili wachezaji wenye uwezo wa kupambana ili kupata matokeo chanya yatakayosaidia kuwafikisha kwenye mipango na mikakati yao.

Na kama timu yako inahitaji kufika hatua ya nusu fainali, fainali au kutwaa ubingwa wa Afrika, hakuna budi viongozi wa klabu husika kuwekeza katika vikosi vinavyofanana na ushindani wa wapinzani ambao wanakutana nao kwenye mashindano hayo ya kimataifa.

Simba, Yanga na timu nyingine za Tanzania ambazo ziko katika vita ya kuwania tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa zinatakiwa kusajili wachezaji ambao wana uwezo na uzoefu wa kupambana kwenye michuani hiyo ya CAF na si kuchanganya 'siasa' na uhalisia wa ushindani uliopo katika kufikia malengo.

Naamini zile kanuni zilizowekwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kuzitaka klabu kusajili wachezaji wa kigeni ambao pia wanacheza katika timu za mataifa wanayotoka, hii itasaidia kuzifanya klabu zetu kuwa imara na zinazocheza soka la ushindani.


Usajili imara ndio njia pekee ya wawakilishi wa Tanzania wanaotaka kutimiza ndoto za kutwaa ubingwa wa Afrika zitatimia na kuwapa furaha mashabiki wa soka wa nchini ambao wanalisubiri taji hilo kwa hamu.

Mbali na kufanya usajili bora, klabu zinatakiwa kuajiri makocha wenye uwezo mkubwa wa kuwavusha na kuwapeleka kule wanapohitaji kufika, kuendelea kusajili wachezaji wa bei rahisi au wa madaraja ya pili, haitakuwa suluhisho la kufikia malengo ya kubeba ubingwa wa Afrika.

Katika kuhakikisha juhudi za kuwekeza kwenye michezo zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, huu ni wakati wa viongozi wa klabu kusajili nyota wenye uwezo na kumaliza 'tetesi' zilizopo za 'upigaji' wa fedha kwenye mchakato huo muhimu kwa maslahi ya maendeleo ya soka Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Timu za Bongo ziwe makini usajili FIFA usiwaletee balaa

Na Adam Fungamwango

**KLABU** ya Yanga imefungiwa kufanya usajili wa wachezaji wa ndani na nje ya nchi.

Imefungiwa kwa sababu ya kukiuka Kanuni ya za Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu (FIFA).

Taarifa hiyo ilitolewa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), Cliford Ndimbo, jana baada ya kupata barua kutoka FIFA ikielekeza hivyo.

Baada ya hapo, TFF, nayo ikapigilia nyundo, nayo ikaifungia Yanga kufanya usajili kwa wachezaji wa ndani.

Sababu iliyotolewa ni kukiuka kile kilichoelezwa ni 'Annexe 3', ya Kanuni ya Uhamisho wa Wachezaji (RSTP) ya shirikisho hilo, ambapo haikuingiza uthibitisho wa malipo ya uhamisho wa mchezaji husika ambaye hakutajwa na TFF katika Mfumo wa Usajili (TMS), licha ya kukumbushwa kufanya hivyo.

Mpaka sasa haijajulikana ni mchezaji gani ambaye alisajiliwa na uthibitisho wa malipo ya uhamisho haikuthibishwa. Si FIFA wala TFF waliomtaja. Waandishi wa habari za uchunguzi wapo katika harakati za kutafuta ni nani kwa sababu wenyewe Yanga wanamfahamu.

Ukiingalia taarifa ile, bado ina maswali mengi ambayo yameachwa. Kijuujuu unaweza kusema imekamilika. Labda TFF imeweka taarifa kifupi sana, ilibidi itoe maelezo ya kujitosheleza.

Taarifa haijasema Yanga imefungiwa muda gani? Kama imefungiwa dirisha kubwa la usajili, je inaweza kufanya chochote kabla ya hapo adhabu hiyo ikaondolewa? Au imefungiwa moja kwa moja?

Ni kama tunavyoona kwa wachezaji na makocha ambao wanadai, klabu inafungiwa kusajili kwa dirisha moja au mawili, lakini inapewa muda kama ikiweza kulipa, basi adhabu hiyo inaendelea. Kwa hili haijaeleza kama kuna kitu kama hicho, badala yake taarifa inasema imefungiwa tu.

Kuna kipengele kinasomeka Yanga inatakiwa kutekeleza matakwa hayo kikanuni na kuwasilisha taarifa kwa Sekretarieti ya Kamati ya Nidhamu ya FIFA ambapo suala hilo limefikishwa kwa ajili ya hatua zaidi.

Hili nalo linachanganya. Je Yanga ikitekeleza matakwa hayo itaondolewa hiyo adhabu?

Je Yanga inatakiwa ifanye kile ambacho imeshindwa kukifanya ili ifunguliwe, au adhabu imesimama pale pale?

Na suala kufikisha katika Sekretarieti ya Kamati ya Nidhamu ya FIFA, ina maana kuna adhabu nyingine zaidi itatolewa? Nadhani haya yote mashabiki wa soka wanahitaji kupata majibu ili suala likae sawa, kwa sababu si tu limewachanganya wanachama na mashabiki wa Yanga, pia limewashtua wadau wa soka nchini.

Nikitoka huko nakuja katika klabu yenyewe ya Yanga. Nadhani imekuwa na matatizo mengi ya kiusajili dhidi ya wachezaji na makocha wake.

Mara kwa mara imekua na mizozo kiasi FIFA inaibuka na kutaka iwalipe, na kwa bahati nzuri inafanya hivyo, maisha yanaendelea.

Kwa hili nawashauri viongozi wa Yanga ambao kwa upande mwingine wanafanya vyema katika masuala ya kusimamia klabu, lakini kwa hili linaweza kuwaletea shida.

FIFA huwa hawaangalii ukubwa na timu, hata vigogo kama Barcelona, Real Madrid, Chelsea zimejikuta zikikumbwa na adhabu kama hiyo.

Yanga isidhani ukubwa ilionao Tanzania na siasa zetu za mpira wa Bongo ndiyo zinaweza kufanya kazi mpaka huko.

Linapokuja suala la FIFA au CAF viongozi wa Yanga wanatakiwa wawe makini, vinginevyo ipo siku wanaweza kujikuta wanaiingiza klabu katika matatizo makubwa.

Na hii nairudia tena kwa klabu nyingine za Tanzania. Ziwe makini sana katika mikataba ya makocha, wachezaji na uhamisho na vitu vingine vinavyofanana na hivyo, ikiwamo hata 'kuchezacheza' na mitandao ya TMS.

TFF nao ifanye 'siasa' zake kwa Simba na Yanga hapa hapa, lakini linapokuja suala la masuala ya usajili ambayo yanahusisha CAF na FIFA wawe wakali, kwa sababu kitendo cha kukubali 'ujanja' wa klabu hizi, ipo siku tunaweza kushuhudia timu moja, au nchi inafungiwa.

TFF inatakiwa itoe semina kwa klabu na kabla ya kukamilisha usajili, yenyewe ijiridhishe na kukataa kila aina ya propaganda au ubaya itakayopewa, ili mradi tu kuilinda klabu isipate madhara na soka la nchi kwa ujumla.

HABARI KITAIFA

# Vurugu zakwamisha uchaguzi CHADEMA

**Na Francis Godwin,** IRINGA

UCHAGUZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Baraza la Wanawake wa chama hicho (BAWACHA) mkoa wa Iringa, umeshindwa kufanyika baada ya kuibuka vurugu.

Vurugu hizo ziliibuka baada ya kuwapo madai kuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Mchungaji Peter Msigwa, alikuwa anapanga safu yake ya uongozi.

Kutokana na vurugu hizo zilizozuka juzi majira ya saa 3:00 usiku kwenye ukumbi wa Gentle Hill mjini hapa polisi walifika na kuwatawanya wajumbe ili kuepusha maafa.

Vurugu hizo zilianza baada ya kuanza uchaguzi wa Baraza la Wazee wa Chadema kutokana na Alex Kimbe, Meya wa zamani wa Manispaa ya Iringa na wajumbe wenzake wawili, kuzuiwa kupiga kura kwa madai si wajumbe halali.

Kimbe ambaye anadaiwa anatoka kambi ya William Mungai, mwenyekiti anayemaliza muda wake, aliwekewa pingamizi la umri baada ya kudaiwa kudanganya umri na kuonyesha amefikisha miaka 50 ya kikanuni jambo ambalo si kweli.

Hali hiyo iliibua vurugu nje na ndani ya ukumbi kutokana na barua ya pingamizi kutolewa dakika za mwisho ukumbini na Mchungaji Msigwa ambae kimsingi kwenye uchaguzi huo alikuwa mtazamaji na si msimamizi.

Baadhi ya wanachama wa CHADEMA waliozungumza na Nipashe nje ya ukumbi, walisema wanashangazwa kuona Msigwa akiingilia uchaguzi huo kinyume cha utaratibu wa chama taifa kwa kuwa hakupangwa kuwa msimamizi.

Walisema alichofanya Msigwa ni kuvuruga uchaguzi baada ya kuona kambi yake inalemewa, hivyo kuanzishwa mizengwe ya kuwakata majina wagombea wenye sifa na kufanikiwa kisha kuanza kuwatoa wajumbe wenye sifa ya kupiga kura.

Katika mahojiano na mwandishi wa habari hii, Kimbe alisema anashangazwa na pingamizi alilowekewa na Mchungaji Msigwa na kutumiwa kwa simu wakati hadi anafika ukumbini, alitambua kuwa ana sifa zote kuwa mjumbe kwenye uchaguzi huo wa wazee.

Alisema kitendo cha kumwondoa kupiga kura ni kufifisha nguvu ya kambi yake ambayo mgombea wake alikuwa Elikus Ngweta ambaye alishinda kwa kura 9 dhidi ya Charles Ndenga aliyepata kura 8 katika nafasi ya mwenyekiti.

Katika uchaguzi wa nafasi ya mwenyekiti wa CHADEMA mkoa, wagombea walikuwa Wakili Emmanuel Chengula na mwenyekiti anayemaliza muda, William Mungai. Hata hivyo, msimamizi wa uchaguzi huo, Catherine Runge, hakuzungumzia hatma ya uchaguzi huo ambao haukufanyika.

Mungai hakutaka kabisa kuzungumzia vurugu zilizojitokeza wala mchakato mzima wa uchaguzi huo huku akisema ni mapema kusema chochote.

Naye Mchungaji Msigwa ambaye alituhumiwa kuvuruga uchaguzi huo, akizungumza kwa njia ya simu, alisema hahusiki na vurugu hizo kwa kuwa hakuwa mgombea.

Katika uchaguzi wa nafasi ya Baraza la Vijana wa CHADEMA (BAVICHA) Mkoa, Nector Kitiga alimshinda kwa kura 13 Vitus Nkuna aliyepata kura tisa.



Baadhi ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), mkoa wa Iringa, wakijadiliana jambo nje ya ukumbi wa Gentle Hill, mjini Iringa juzi, baada ya uchaguzi wa viongozi ngazi ya mkoa kuvurugika kutokana na vurugu kubwa iliyotokea. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mpango mgeni rasmi miaka 102 ya Nyerere

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KONGAMANO la kumbukizi ya miaka 102 kuzaliwa kwa Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, linatarajiwa kufanyika leo jijini hapa ili kuwahimiza vijana kumuenzi kwa kulinda na kudumisha amani.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapa, Mkuu Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema kongamano hilo limeandaliwa na Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

"Kongamano linalenga kuwajenga vijana kumuenzi Baba wa Taifa kwa kazi nzuri ya kujenga na kudumisha amani, kushiriki kwake katika ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika, uhifadhi wa mazingira na maliasili za taifa," alisema.

Alisema taasisi hiyo imeendaa mdahalo kuhusu umuhimu wa kudumisha amani na mshikamano wa kitaifa kwa kuongozwa na kaulimbiu isemayo: 'Kudumisha Amani ni Haki na Wajibu Wetu kwa Maendeleo Endelevu ya Taifa Letu'.

Pia alisema taasisi hiyo itampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa miaka mitatu ya uongozi wake kwa kudumisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa sambamba na maadhimisho miaka 60 ya Muungano.

"Tutampongeza Rais kwani kwa kauli mbiu yake ya kazi iendelee tumeshuhudia akiendeleza mambo mengi ambayo pia Baba wa Taifa aliyaanzisha," alisema.

Senyamule alisema viongozi na mabalozi kutoka nchi mbalimbali watahudhuria kongamano hilo na kutoa wito kwa wananchi kujitokeza kumkumbuka Mwalimu Nyerere ambaye ameliachia taifa amani, upendo na moyo wa kujenga nchi kwa uzalendo.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Peter Mavunde, alisema tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo ina miaka mitatu na imekuwa ikifanya maadhimisho hayo na makongamano yenye lengo la kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa kuwa na mpango mkakati wa kuwarithisha vijana mambo yaliyofanywa na muasisi huyo.

"Kwa mwaka huu mada kubwa ni umuhimu wa kutunza amani kwa maendeleo ya taifa na katika shughuli hii tutamuenzi Baba wa Taifa kwa falsafa ya kuasisi utunzaji wa maliasili za taifa pamoja na utunzaji wa mazingira," alisema.

# TARURA yajitia kitanzi kuhusu ubora barabara

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKALA ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), umedhamiria ifikapo mwaka 2025/26, asilimia 85 ya mtandao wa barabara wa kilometa 144,429,077 unaozihudumia zinapitika muda wote.

Mtendaji Mkuu wa TARURA, Mhandisi Victor Seff, alisema hayo jana mjini hapa wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa TARURA cha kuipitia bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 ambayo itawasilishwa bungeni mwezi ujao .

Mhandisi Seff alisema, lengo kuu la mkakati huo ni kuhakikisha barabara hizo zinapitika wakati wote ili kuchangamsha uchumi na kuwezesha upatikanaji wa huduma za kijamii na za kiuchumi kwa urahisi.

Alisema kwa sasa zaidi ya kilometa 100,000 za barabara ni za udongo na ndizo zenye shida kubwa zinaponyesha mvua hata kwa kwiango kidogo na kusababisha nchi nzima inakuwa kama imesimama.

Mhandisi Seff alisema asilimia 44 uliyobakia barabara zake ndizo zenye mtandao uliokuwa mzuri zikiwamo za lami zaidi ya kilometa 3,200 na barabara za changarawe zaidi ya kilometa 41,000 . alisema kufanyika kwa baraza hilo ni hatua ya kuwashirikisha wafanyakazi ili waweke michango yao kwenye bajeti hiyo.

"Vikao hivi vya baraza vina lenga kuwashirikisha watumishi katika uendeshaji wa taasisi na katika uboreshaji wa maslahi yao ili kuwezesha kufikia lengo letu " alisema Mhandisi Seff.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Migodini, Kazi za Ujenzi (TAMICO), Paternus Rwechungura, aliishauri tarura husussani wahandisi na wataalamu wanaoshughulika na ujenzi wasisite kujinga na chama cha wajenzi ili washirikiane na wenzao wakiwemo wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) katika kubadirishana uzoefu wa sekta ya ujenz

Alishauri wakala uendelee kuziangalia na kukarabati barabara zilizoko vijijini na mijini ili kuwezesha utoaji wa huduma za usafiri na usafirishaji kuwa bora na wa kuaminika nyakati zote .

Mwakilishi wa Kamishna wa Kazi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu , Kazi, Vijana , Ajira na Wenye Ulemavu , Tulia Msemwa, aliwashauri wajumbe wa baraza hilo kutoa maoni na mapendekezo yao katika bajeti hilo ili kuhakikisha wakala huo unafikia malengo , dhima na dira iliyojiwekea . Msemwa ambaye ni Ofisa Elimu Kazi Mwandamizi kutoka ofisi hiyo, alisema TARURA imejiwekea mipango mbalimbali hasa kuboresha miundombinu ya barabara ambayo itaisaidia kutatua changamoto na kufikia kwenye ufanisi wenye tija na malengo mazima yaliyowekwa na taifa.

# Mpango kabambe matumizi nishati safi kupikia

**Na Joseph Mwendapole**

WIZARA ya Nishati imesema imeweka mikakati kuhakikisha ifikapo mwaka 2033 asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema hayo jana wakati akizungumzia maonyesho ya sekta ya nishati.

Maonyesho hayo yanatarajiwa kuanza keshokutwa na yatafanyika kwa siku tano katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma.

"Wizara imeamua kwa dhati kabisa kulibeba suala la nishati safi ya kupikia kama ajenda maalum ili kuwawezesha Watanzania kuondokana na matumizi ya nishati isiyo safi na wahamie kwenye matumizi ya nishati safi," alisema.

Biteko alisema kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani miaka ya karibuni, bei ya mafuta imeendelea kupanda na kufanya matumizi ya fedha za kigeni kuwa makubwa kwa ajili ya kuagiza nishati hiyo.Alisema wizara ina mikakati kabambe ya kupunguza utegemezi wa mafuta, hivyo nia ni kuhimiza matumizi ya gesi asilia kuendesha magari na mitambo inayotumika viwandani.

Biteko alisema maonyesho hayo yamekuwa yakiwapa fursa ya kuonyesha dira na mwelekeo wa sekta ya nishati na kwamba mwaka huu ajenda kuu ni nishati safi ya kupikia ambayo imemng'arisha Rais Samia Suluhu Hassan katika bara zima la Afrika.

Desemba 2, mwaka jana, Rais Samia alizindua mradi wa nishati safi ya kupikia itakayowasaidia wanawake barani Afrika katika mkutano uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kando ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28).

Biteko alisema maonyesho hayo ni fursa kwa wabunge na watanzania wengine kufahamu utekelezaji wa sera ya nishati kwa mwaka 2024/25 na mwelekeo wa sekta hiyo katika kukuza uchumi wa nchi.

Alisema Wizara ya Nishati ambayo imepewa wajibu wa kusimamia masuala ya umeme, mafuta, gesi na utafutaji wa gesi kwenye maeneo mbalimbali nchini, imekuwa na kawaida ya kufanya maonyesho hayo kila mara wakati wa Bunge la Bajeti. "Tumekuwa na utaratibu huu wa kukutana na wadau wetu kila mwaka kutupa maoni ya maeneo ya kufanya maboresho na waseme maeneo ambayo wanaona tunafanya vizuri pia," alisema Biteko.

Aidha, alisema kwa miaka yote ambayo wizara imekuwa ikifanya maonyesho hayo kumekuwa na mafanikio makubwa kwa wadau kuibua hoja ambazo zimekuwa zikifanyiwa kazi ikiwemo kutoa ufafanuzi kwa mambo ambayo hayakuwa yakifahamika.



Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam, wakiangalia vazi la kanzu za mtumba kabla ya kuzinunua katika Mtaa wa Kongo, eneo la Kariakoo, mapema wiki hii. Kanzu moja iliuzwa kwa bei ya 5,000/- hadi 7,000/- kulingana na ubora wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Taasisi zaagizwa kushiriki kutatua changamoto ya wanyama waharibifu

**Na Ashton Balaigwa,** MVOMERO

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, imeagiza taasisi zilizoko chini ya wizara hiyo kushirikiana na viongozi wa wilaya zote nchini kutatua tatizo la wanyamapori wakali na waharibifu.

Lengo la kufanya hivyo ni kupunguza migongano kati ya binadamu na wanyamapori katika vijiji vinavyozunguka hifadhi na mapori ya akiba.

Naibu Waziri wa Malisili na Utalii, Dunstan Kitandula, aliytoa agizo hilo juzi katika mkutano na wananchi wa vijiji vya Mangae, Doma na Mkata, Mvomero mkoani Morogoro wakati wa operesheni ya kurudisha kundi la tembo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Operesheni hiyo ilifanyika kwa kutumia helikopta ambayo ilifanikisha kundi la tembo 45 waliokuwa maeneo ya makazi ya wananchi wa vijiji hivyo kuswagwa na kurejeshwa kwenye hifadhi hiyo.

Kitandula alisema,lengo la kuwarejesha tembo hao hifadhini ni jitihada zinazofanywa na serikali katika kuwahakikishia usalama wananchi ili kupunguza migangano hiyo kati ya binadamu na wanyamapori na kuwapo uhifadhi endelevu kwa faida ya nchi.

"Tunatumia helikopta katika zoezi hili na limetumia gharama kubwa,. Licha ya ukubwa wa gharama hizi serikali lengo lake ni kupunguza migongano na kero kwa wananchi wa maeneo haya ambao kadhia za wanyama zimekuwa zikihatarisha usalama na mali zao, " alisema Kitandula.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, aliipongeza serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuwezesha kuwarejesha tembo hao kwa kutumia helikopta kwa kuwa changamoto ya wanyamapori hususani tembo ni ya muda mrefu kwa wananchi wa vijiji hivyo.

Kwa mujibu wa mkuu wa wilaya,kata tano zinazokabiliwa na tishio la wanyamapori waharibifu ni Doma, Mangae, Msongozi , Lubungo na Melela ambazo baadhi ya vijiji viko karibu na Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Mbunge wa Mvomero, Jonas Zeeland, alisema uwezeshaji wa kurejesha wanyamapori hao ni faraja kwa wananchi kwa vile tembo wamekuwa wakisababisha uharibifu mkubwa wa mali na kuhatarisha uhai wa wananchi.

"Kwa kweli naipongeza serikali kwa kusikia kilio cha wananchi na kuchukua hatua baada ya kupeleka mapendekezo bungeni na kwa Waziri wa Maliasili na Utalii," alisema Zeeland.

Awali, Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Dk. Eblate Mjingo, alisema taasisi hiyo imeendelea kubuni mbinu mbadala za kutatua migongano kati ya binadamu na wanyamapori nchini hususani tembo.

Naye Juma Omary, mkazi wa kata ya Doma, alipongeza serikali kwa kuwasaidia kuondoa makundi hayo ya tembo katika maeneo yao licha ya kuwa yalikuwa tishio katika uhai wao lakini yalikuwa yakifanya uharibifu katika mashamba yao

# Mbunge apongezwa kwa kuwakutanisha wananchi

**Na Munir Shemweta,** MLELE

MBUNGE wa Kavuu katika Halmashauri ya Mpimbwe mkoani Katavi na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amepongezwa kwa kuwakutanisha wananchi wa jimbo lake kusheherekea nao sikukuu ya Eid El Fitri jambo lililoelezwa kuwa linaleta umoja na ushirikiano.

Pongezi hizo zilitolewa juzi wakati wa Eid Pili katika hafla iliyoambatana na chakula cha mchana, iliyofanyika nyumbani kwake, Kibaoni wilayani Mlele na kujumuisha watu mbalimbali akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Alhaji Majid Mwanga.

Wakizungumza wakati wa hafla hiyo, viongozi mbalimbali wakiwamo wa dini, walitoa pongezi kwa mbunge huyo kwa uamuzi wake wa kuwakutanisha waumini wa Kiislamu na wananchi wengine kwa ajili ya kusherekea sikukuu ya Eid El Fitri.

Katika historia ya jimbo hilo, walisema hiyo ni mara ya kwanza kufanyika hafla ya aina hiyo na kwamba si tu iimeleta umoja na ushirikiano bali faraja kwa wananchi na kuonyesha kwamba mbunge wao yuko karibu nao.

Alhaji Mwanga alisema watumishi wa umma katika wilaya, wanayo faraja kubwa ya kuwa na mbunge katika hafla ya kusheherekea sikukuu ya Eid Pamoja. Aliweka bayana kuwa watafanya kila linalowezekana ndoto, matamanio na mahitaji waliyo nayo wananchi kwake yanatimia.

"Kazi ambayo tunapaswa kuifanya ni kuwasemea mambo mazuri ili kuongeza moyo na ari ya kufanya kazi zaidi," alisema Alhaji Mwanga

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mlele, Wolfgang Mizengo Pinda, alipongeza uamuzi uliofanywa na nbunge huyo na kwamba jambo hilo limejenga mhimili wa kuimarisha uhusiano baina ya wananchi wa madhehebu tofauti ya dini.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mpimbwe, Shamim Mwariko, alisema wanapopatikana viongozi wanaojitambua na kusimamia majukumu yao ipasavyo, kuna wajibu wa wananchi kumshukuru Mungu, kuwafuata pamoja na kuwaombea kwa Mungu.

Akimwakilisha Sheikh wa Mkoa wa Katavi, Sheikh wa Wilaya ya Tanganyika, Ayoub Mfutakamba, alimshukuru Naibu Waziri Pinda kwa kuwakutanisha wananchi wa Mpimbwe huku akimpongeza kwa kazi nzuri anayoifanya katika wizara anayoiongoza hususan kutatua migogoro ya ardhi kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo katika mkoa wa Katavi.

Naibu Waziri Pinda aliwaomba wananchi wa Mpimbwe kuendelea kumuombea kwa Mungu wakati wa kutekeleza majukumu yake.

"Ni kazi kubwa sana kuongoza watu kwa sababu wewe huna maarifa yanayowazidi na wakati mwingine wao wana maarifa yanayokuzidi," alisema.

Aliwataka waumini wa Kiislamu na wananchi wa Kavuu kwa ujumla kuwa karibu naye sambamba na kumtumia katika kuleta maendeleo ya jimbo kwa kuwa yeye yuko katika nafasi hiyo kama mwajiri wao.





# Wahabesh jela miezi 18 kuingia bila kibali

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Manyara, imewahukumu wahamiaji haramu 20 raia wa Ethiopia, kutumikia kifungo cha mwaka mmoja na nusu kila mmoja au kulipa faini Sh. milioni moja kila mtu kutokana na kosa la kuingia nchini bila kufuata taratibu za kisheria.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Martine Masaho, alisema washtakiwa hao walikamatwa Machi 23, mwaka huu, katika kizuizi cha polisi Minjingu, wilayani Babati mkoani Manyara wakisafirishwa kwenda Afrika ya Kusini.

Aidha mshtakiwa wa pili hadi wa 20, walipewa nafasi ya kujitetea na wote walikiri kwa nyakati tofauti kuingia nchini bila kufuata taratibu za kisheria.

Baada ya kukiri waliiomba mahakama kuwapunguzia adhabu kutokana na kosa walilolifanya.

Wakati wao wanahukumiwa mshtakiwa namba moja, dereva aliyekuwa akiwasafirisha, Edward Erihard, kesi yake itatajwa Aprili 30, mwaka huu, kutokana na kukana mashtaka na ataendelea kuwa nje kwa dhamana.

Naye Wakili wa Serikali, Rose Kayumbu, aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaokiuka sheria.

Hakimu Masaho baada ya kusikiliza pande zote mbili aliwatia hatiani kwenda jela kutumikia kifungo cha mwaka mmoja na nusu kila mtu au kulipa faini ya shilingi milioni moja kila mtu.

Waethiopia hao na dereva aliyekuwa akiwasafirisha, walisomewa mashtaka Machi 28, mwaka huu.

Awali, Hakimu alianza mapema kusikiliza kesi hiyo lakini iliahirishwa kwa muda baada ya mkalimani aliyekuwa akitafsiri lugha ya kiethiopia, mawasiliano yake kukatika na baadaye yaliporejea, kesi iliendelea.

# Bosi wa TEHAMA ahadharisha madhara matumizi yasiyo sahihi mifumo kidijitali

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

TUME ya TEHAMA Tanzania (ICTC), imesema kutokuwapo kwa matumizi sahihi ya mifumo ya kidijitali, kunaweza kusababisha kutwezwa kwa utamaduni wa taifa na utu wa Watanzania.

Hatua hiyo ni kutokana na kuruhusu taarifa za siri za serikali, kampuni na za mtu binafsi kupatikana kwa utaratibu usio sahihi; kisha kutumiwa na watu wasiokuwa na dhamana ya kutumia taarifa husika.

Pia imesema dhana ya mabadiliko ya tabia za binadamu na matumizi ya teknolojia za kidijitali, haziwezi kufanikiwa endapo mifumo ya kidijitali, itakuwa kikwazo kwa ukuaji uchumi na ukuaji wa biashara za kampuni na shughuli za mtu mmoja mmoja.

Mkurugenzi Mkuu wa ICTC, Dk. Nkundwe Mwasaga, alisema hayo juzi jijini hapa katika jukwaa la tatu la usalama wa mitandao linalowashirikisha wataalam, watunga sera na viongozi wa viwanda.

Alisema malengo ya mageuzi ya kidijitali, hayawezi kufikiwa endapo suala la usalama wa mitandao linalowezesha matumizi salama ya huduma za kidijitali, halitapewa uzito unaoendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA).

Jukwaa hilo lililowashirikisha wadau 350 kutoka kampuni mbalimbali, washirika wa maendeleo na mashirika yasiyo ya kiserikali, lilichagizwa na mada kutoka kwa Mshauri wa Ulinzi wa Taarifa kutoka Ujerumani, Dk. Tino Naumman na Mshauri wa Serikali wa Masuala ya Mitandao wa Estonia, Margus Magi.

Tanzania inashika nafasi ya pili barani Afrika, nyuma ya Mauritius, kwa kuwa kinara wa masuala ya usalama wa mtaandao,

Kaulimbiu ya mwaka huu inasema 'Kutengeneza Dunia ya Mtandao Iliyo Jumuishi na Shirikishi'.

"Sote tunafahamu kwa suala la mageuzi ya kidijitali ni endelevu na mtambuka, hivyo sote kwa pamoja hatuna budi kuendelea kuchukua hatua za makusudi za kutunga na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na mikakati inayolinda usalama wadau wote walio katika ikolojia ya kidijitali (Digital Ecosystem) kuanzia serikali mpaka mtu mmoja mmoja.

"Umadhubuti wa mfumo wa kisheria, utajengwa na maendeleo ya ubunifu wa mbinu mbalimbali za kitaalamu za kuhakikisha kuwa Tanzania iko katika ulimwengu wa kidijitali ulio salama.

"Usalama wa mtandao una mahusiano makubwa na uwekezaji; ambapo kwa Tanzania tumeanza kupata mafanikio makubwa katika uwekezaji kutokana na juhudi zinazoendelea katika usalama wa mtandao," alisema.

Kuhusu matumizi ya akili mnemba, Dk. Mwasaga alisema kuwa teknolojia hiyo haiwezi kufanya kazi bila kupata taarifa.

Katika jukwaa hilo, Mwenyekiti wa Bodi ya ICTC, Prof. Leonard Mselle, alisema ufundi wa kidigiti kwa kwa sasa ndio ufundi mkubwa kuliko ufundi wowote ule duniani, ambao umesababisha kugunduliwa kwa teknolojia ya akili mnemba (AI).

" Tanzania kama sehemu ya dunia, hatuwezi kuacha kujijengea uwezo katika kuelekea uchumi wa kidigiti, kwa kuwa dunia nzima inaelekea humo ikiwa ni pamoja na kutoa huduma mbalimbali, zikiwemo za kijamii, kiserikali na binafsi," alisema.

Mkufunzi wa TEHEMA kutoka Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), Sakina Seleman, alisema jukwaa hilo la siku mbili lina umuhimu mkubwa, hasa kwa wanawake kutokana na changamoto kubwa iliyopo kwa sasa ya masuala ya ukatili wa kimtandao kwa wanawake.

"Mimi kama mtaalam wa masuala ya mtandao tumepata fursa nzuri kupitia Jukwaa hili ya kujadili kwa kina jinsi ya kufanya mtandao iendelee kuwa salama katika nchi yetu pamoja na watumiaji," alisema.

Jumatano wiki hii, wakati Rais Samia Suluhu Hassan anazindua Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, alitoa miezi sita pamoja na maelekezo matano kwa Wizara husika na taasisi za umma, kuhakikisha mifumo ya TEHAMA iwe imesomana.

Aliagiza tume hiyo kuhakikisha taasisi zote za umma na binafsi zinasajiliwa na kutekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kabla ya mwezi Disemba mwaka huu.




Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki (kulia), akizungumza baada ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Batilda Burian (katikati), kuwasili wilayani humo jana, kwa ajili ya ziara ya kukagua miradi itakayopitiwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru. Wengine ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina (kushoto) na (wapili kushoto) ni Mkuu wa wilaya hiyo, Zainabu Abdallah. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Hatima ya kesi ya Pauline Gekul Aprili 15

**Na Godfrey Mushi,** BABATI

HUKUMU ya kesi ya rufani iliyofunguliwa na Hashim Ally katika Mahakama Kuu, Kanda ya Manyara, dhidi ya Mbunge wa Babati Mjini (CCM), Pauline Gekul, imepangwa kutolewa Aprili 15, mwaka huu.

Gekul anakabiliwa na kesi ya unyanyasaji dhidi ya aliyekuwa mfanyakazi wake, Hashim Ally.

Kwa mujibu wa hati ya wito ya kuitwa shaurini Wakili wa Hashim Ally, Peter Madeleka, hukumu hiyo itasoma saa 8:00 mchana Aprili 15, mwaka huu na Jaji Devota Kamuzola anayesikiliza kesi hiyo.

Mwezi uliopita, mahakama hiyo ilisikiliza mapingamizi matatu ya upande wa utetezi katika kesi hiyo.

Mapingamizi hayo yaliwasilishwa katika mahakama hiyo na Wakili Ephraim Kisanga anayemwakilisha Gelul katika shauri hilo la rufani ya jinai, namba 577 ya mwaka 2024.

Pingamizi la kwanza lilikuwa la mahakama hiyo kukosa mamlaka ya kisheria ya kusikiliza rufani iliyotolewa na mrufani Hashim Ally.

Kwa mujibu wa Wakili Kisanga, pingamizi lao la pili ni kwa mtoa rufani, alishindwa kutafuta njia nyingine mbadala ya kisheria tofauti na rufani.

Pingamizi la tatu ni kuhusiana na notisi (ilani) iliyotumika kufungulia kesi ya msingi, ambayo ni rufani namba 577, ilikuwa haikidhi vigezo vya kisheria kuitwa notisi.

Mrufani katika kesi hiyo Hashimu Ally, anawakilishwa na Wakili Peter Madeleka, anayesaidiwa na Wakili Thadey Lister na John Masanja.

Aidha katika shauri la msingi, Gekul alikuwa akikabiliwa na shtaka moja la shambulio na kusababisha madhara kwa mwili, chini ya kifungu cha 241 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, Marekebisho ya Mwaka 2022.

Alikuwa anadaiwa kuwa yeye na watu wengine ambao hawako katika malalamiko hayo, Novemba 11, 2023 mjini Babati, mkoani Manyara, walimwita Hashim na kumweka kizuizini.

Pia wanadaiwa kumtishia kwa silaha ya moto, kumvua nguo na kumshambulia kwa kumlazimisha kukalia chupa ya soda ili iingie katika njia yake ya haja kubwa.



# Othman achagiza umuhimu maadili

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni muhimu kwa jamii kuendeleza utamaduni wa kuwalea watoto kwa kuzingatia misingi na miongozo ya dini.

Othman aliyasema hayo juzi Matemwe wilaya ya Kaskazini A, Unguja, alipozungunza na wananchi, wazee, walimu na wanafunzi wa madrasa za kijiji hicho baada ya kuzindua rasmi Jumuiya ya Maendeleo ya Kiislamu ya Matemwe.

Taasisi hiyo, pamoja na mambo mengine, ina jukumu la kuendeleza na kutunza mila, desturi na maadili.

Alisema wazee Matemwe wanastahili kuwa alama na mfano sambamba na darasa la mafunzo kwa watu wengine wa Zanzibar kujifunza walivyobuni utaratibu bora wa kuwasaidia watoto kuendeleza kukua katika mila na maadili mema.

Aliwapongeza wazazi na waalimu wa madrasa za kijiji hicho kwa kukubali kuendeleza malezi bora katika kuwalea watoto wa wao jambo ambalo linapaswa kuungwa mkono na watu wengine.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A, Othman Ali Maulid, alisema serikali ya mkoa Kaskazini Unguja inaunga mkono juudi za wazazi na walimu wa madrasa wa kijiji hicho katika kuwalea watoto kwa misingi bora.

Alizishauri shehia zingine zilizoko ndani ya wilaya hiyo kuiga mfano wa wenzao wa Matemwe katika kuwalea, kuwajenga na kuwakuza watoto kiimani na kimaadili jambo ambalo litasaidia katika kupata watoto bora wenye udustawi wa maadili mema.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Ameir Kundi, alisema kwamba jumuiya imepunguza wimbi la mmong'onyoko wa maadili ndani ya kijiji hicho na kuwajenga watoto kuwa na mwelekeo bora wa mafunzo ya dini.

# ZBS yaanza ujenzi maabara za kisasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI ya Viwango Zanzibar (ZBS) imesema inaendelea na miradi ya ujenzi wa maabara tano za kisasa za ukaguzi ikiwamo ofisi na maabara inayojengwa Chamanangwe, Pemba ili kuongeza ufanisi.

Mkurugenzi Mkuu wa ZBS, Yussuph Majid Nassor, aliyasema hayo jana wakati akifungua Jukwaa la Vyombo vya Habari lililoandaliwa na taasisi hiyo kwa uratibu wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC) katika ofisi za makao makuu ya taasisi hiyo, Maruhubi, Mjini Unguja.

Alisema hatua hiyo imelenga kuongeza ufanisi wa taasisi kwenye ukaguzi, udhibiti na uthibitishaji wa viwango vya bidhaa zinazozalishwa na kuingizwa nchini kwa manufaa ya wananchi na mazingira.

Nassor alisema hatua hiyo itapunguza changamoto ya kusafirisha sampuli za bidhaa kutoka Pemba hadi Unguja kwa ajili ya uchunguzi na pia kupata majibu ya haraka. Alisema mradi huo utagharimu Sh. bilioni 6.5.

"Tayari zabuni za ujenzi zimeshatangazwa baada ya kukamilika kwa hatua za awali za ujenzi huo ikiwamo ya usanifu wa michoro. Ujenzi utakapoanza, utachukua miezi 24 hadi kukamilika, hivyo kupanua wigo wa utendaji," alisema. Kuhusu uimarishaji wa majukumu ya taasisi, alisema alisema imeendelea kuimarisha maabara za taasisi hiyo zilizozinduliwa mwaka jana pamoja na kukamilisha hatua za awali za kituo cha ukaguzi wa magari kitakachofunguliwa baadaye mwezi huu.

Pia alisema taasisi ina mradi wa kituo cha magari ambao umegharimu Sh. bilioni 2.5 umekamilika katika hatua ya majengo na wiki ijayo, ufungaji mitambo unatarajiwa kuanza.

Mbali na miradi ya ujenzi, alisema taasisi hiyo pia imepata mafanikio yakiwamo kutambuliwa kimataifa na Shirika la Viwango Duniani (ISO) na baadhi ya maabara zake kupata alama ya ithibati ubora ya mashirika ya kikanda likiwamo la ukanda wa Kusini mwa Afrika.

Makamu Mwenyekiti wa ZPC, Tabia Makame Mohammed, aliipongeza taasisi hiyo inavyofungamana na vyombo vya habari na kuomba taasisi zingine kuiga mfano huo.

Alisema vyombo vya habari ni daraja linanowakutanisha wananchi na taasisi za umma au binafsi hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa pamoja.

Aidha, aliipongeza ZBS kwa kuendelea kupiga hatua za maendeleo ikiwamo kujitegemea kwa asilimia, 100 hivyo kuiondolea serikali mzigo wa uendeshaji jambo linalotokana na usimamizi bora wa ukusanyaji wa mapato na utoaji wa huduma bora.




Ofisa Maabara ya ujenzi wa Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), Salim Kassim Juma (wa tatu kulia), akitoa maelezo kwa waandishi wa habari kuhusu vifaa vya maabara vinavyotarajiwa kufungwa hivi karibuni, walipotembelea taasisi hiyo, Zanzibar jana, ikiwa ni sehemu ya Jukwaa la Viwango la Vyombo vya Habari lililoratibiwa na Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC). **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waagizwa bajeti kuzingatia usawa jinsia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imewataka wakurugenzi wa sera na mipango katika wizara na taasisi za serikali ya Zanzibar, kuzingatia usawa wa kijinsia wanapoandaa bajeti ili kuratibu na kupata kizazi chenye usawa.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Abeda Rashid Abdallah, alisema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha kuwajengea uwezo wakurun gezi wa sera na mipango na baadhi ya maofisa wadhamini wa wizara za serikali ya mapinduzi Zanzibar (SMZ) kilihofanyika visiwani hapa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kufikia malengo ya serikali na dunia katika kuwainua wanawake katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Abeda alisema lengo la kikao hicho ni kuwajengea uwezo wa kujua kizazi chenye usawa na kuratibu utekelezaji wake kitaifa, hivyo aliwataka kutimiza majukumu kwa ufanisi ili kuendelea kuing'arisha Tanzania kimataifa.

Pia alisema wizara zinaelekea katika kipindi cha kuandaa bajeti ya mwaka 2024/25, hivyo ni muhimu kuijua program ya uswa wa kijinsia na kuingiza katika sekta zao hatimaye kutoa ripoti nzuri itakayoisaidia Tanzania katika kufikia hatua hiyo.

Aliwasisitiza kuwa masuala yaliyowekewa ahadi yawamo katika sekta husika na kutoa takwimu sahihi na kwa wakati katika taarifa kuhusu yaliyofanyika katika sekta kama za maji, umeme na kilimo.

Naye Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto, Siti Abbas Ali, aliwataka waratibu wa jinsia katika wizara hizo kusimamia, kupanga na kuingiza masuala ya kijinsia katika sekta zao ili kutoa unafuu katika utekelezaji kwa kuzingatia sheria na kanuni.

Mratibu wa programu ya kizazi chenye usawa kutoka wizara hiyo, Leah Ipini, alisema programu hiyo itamwezesha mwanamke kiuchumi na atashiriki katika kazi mbalimbali zikiwamo za kisiasa, kiuchumi na kijamii na kupata kipato cha kuendesha familia na kuepukana na utegemezi.



**VERA SIDIKA**
UKURASA 13

Nipashe
MWANGA WA JAMII

JUMAMOSI APRILI 13, 2024



# 'WAMEWEZA'

NDOA ya wasanii maarufu wa Bongo Fleva, Nandy na Billnas, inazidi kuimarika na kutajwa kama ya mfano kwa wanamuziki vijana nchini.

Imeelezwa ndani ya zaidi ya mwaka mmoja tangu mastaa hao wafunge ndoa, Nandy na Billnas wamekuwa makini na viashiria vya kuwasambaratisha na kuwafanya waonekane kama wapya kila wakati.

Wasanii hao wenye mtoto mmoja, wamefanikiwa kuyafanya maisha yao kuwa siri na kuhakikisha migogoro yao kubaki ndani.

Baadhi ya mashabiki zao walioshiriki kuweka maoni yao katika video ya Nandy ambayo iliambatanishwa na ujumbe mzito wa kimahaba, walieleza kufurahishwa kwao kuwaona mastaa hao wakiwa pamoja, jambo ambalo wengine waliishia njiani.

Nandy katika ujumbe wake, alimsifia mume wake kwa kumpatia furaha kila wakati na kuyafanya mapungufu yao kuwa raha ya maisha yao.

"Mume wangu kipenzi nina furaha kwakuwa tunaendelea kukua pamoja. Asante kwa kuwa mume wangu, asante kwa kuweka tabasamu usoni mwangu kila iitwayo leo! Mapungufu yetu ndo furaha yetu ya kujuana na kupendana zaidi, sina cha kukuahidi zaidi ya kuku-omba tuendelee kupiga Goti pamoja ili tuendelee kuona na kusherekea miaka ikiongezeka pamoja mpaka uzeeni," umsema ujumbe huo.

Waliochangia ujumbe huo walionekana kuvutiwa na maisha yao na kuwataka kuendelea kuilinda ndoa yao na kuondoa dhana kwamba watu maarufu hawawezi kuishi ndani ya ndoa kwa muda mrefu.

BASI SAWA

## Simon Kulwa amshukuru Mungu



Baada ya kuimba kwaya ya Chang'ombe kwa muda mrefu, mwimbaji Simon Kulwa ameamua kutoka kivyake na wimbo unaoitwa Baba Nitakushukuru.

Akizungumza na BT, Simon amesema kutoa wimbo huo kwake ni hatua kubwa kwa sababu ameamua kujitegemea kama mwimbaji binafsi na anashukuru wimbo huo mpya umepokewa vizuri.

"Kupitia wimbo huu mpya nimeishauri jamii kwamba tumshukuru Mungu kwa kila jambo maana yeye ndio anatupa maisha yetu kila wakati. Nimemua kumwimbia Mungu nikiwa binafsi na wimbo wangu unapatikana kwenye mitandao yote," amesema Simon Kulwa.

## Hatimaye Marioo amkaribisha mtoto

HATIMAYE mwanamuziki maarufu wa Bongo Fleva, Marioo, ametangaza hivi karibuni anatarajia kupata mtoto na mpenzi wake Paula Kajala.


Awali kulikuwa na tetesi kwamba Kajala ana ujauzito na wawili hao wanatarajia kupata mtoto wao miezi michache inayokuja.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Marioo aliweka video fupi na kuandika ujumbe ambao umemaliza utata na tetesi juu ya ujauzito wa mpenzi wake Paula Kajala baada ya kuchapisha Video fupi kwenye ukurasa wake akisemTutaongeza mwanachama mpya kwenye kikosi chetu hivi karibuni




Inshallah! Najivunia wewe Malkia wangu Paula Kajala. Mungu akubariki wewe na Familia hakuna matata".

Mama wa Paula Kajala Frida akaweka comment na kuandika "Mkweee".



# UKIMYA NI DAWA TOSHA

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, amesema hawezi kujibu kila kitu kinachosemwa na wasanii aliowatoa, kwa sababu kufanya hivyo ni kutokomaa kisanii.

Amesema kila msanii anayetoka katika mikono yake anaweza kusema kila kitu, lakini moyoni mwake anajua nini amemfanyia katika maisha yake ya muziki hadi alipo kwa sasa.

"Wasanii wote wanaopitia mikononi mwangu wanaweza kusema hiki au kile, kwa upande wangu siwezi kujibu, hata nikisikia nini nakaa kimya kwa sababu hata huyo anayezungumza moyoni mwake anajua nini nimemfanyia mpaka hapo alipo," amesema Diamond.



# Vera apambana na wanaomkera

MPAMBAJI wa video za muziki na jasiriamali, Vera Sidika amesema hawezi kula matapishi yake kwa kurudiana na baba watoto wake, Brown Mauzo.

Vera Sidika ameonekana kukerwa na baadhi ya mashabiki wake kufananisha mchoro wa tattoo alionao na ule uliopo kwenye mwili wa Brown Mauzo.

Amewataka watu wenye mawazo kama hayo kuacha mara moja kwa sabubu michoro hiyo haiwezi kufutika na haina maana mpezni wake huyo wa zamani huko moyoni mwake.

## BURIANI MJELAJELA MALU STONCH

**Na Adam Fungamwango**

TASNIA ya muziki nchini ilipata pigo kubwa Jumamosi iliyopita ilipompoteza mmoja wa wanamuziki wakubwa, mwenye sauti nyororo, Malu Stonch.

Mwanamuziki huyo aliyetokea Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na kuingia nchini mwanzoni mwishoni mwa miaka ya 1990, alifariki dunia kwa kuanguka akiwa jukwaani, akiwa anaimba.

Ni mmoja wa wanamuziki waliovuma wakiwa na bendi za FM Academia na Stono Musica.

Hizi ni bendi pacha, kwani Stono Musica iliundwa na wanamuziki waliojiengua kutoka FM Academia, akiwemo yeye mwenyewe Malu.

Mwanamuziki huyo ambaye alipenda sana kuwa na rasta kichwani, alitarajiwa kuzikwa leo jijini Dar es Salaam.

Hizi ni baadhi ya nyimbo tano ambazo ametunga na zingine kushiriki kuimba akiwa na bendi hizo mbili alizozipigia wakati wa uhai wake.

### Prison

Wimbo huu ulijichukua umaarufu mkubwa ulipofyatuliwa mwanzoni mwa miaka ya 2000.

'Prison' ni wimbo uliibeba jina la albamu hiyo iliyotikitisa, ambao ulizungumzia visa na mikasa iliyowapata wakati baadhi ya wanamuziki wa bendi ya FA Academia wakiwa gerezani, walipokamatwa kwa sababu za kasoro za kiuhamiaji, wakiishi nchini wakati vibali vya vikiwa vimeisha muda. Malu alikuwa mmoja wa walioimba wimbo huu.

### Dotnata

Malu pia aliimba wimbo wa 'Dotnata' ambao ulikuwa kwenye albamu hiyo hiyo ya 'Prisons', na kuufanya kupendwa mno na mashabiki wa bendi hiyo na muziki kwa ujumla.

### Hadija

Kwa masikitiko makubwa huu ndiyo wimbo wa mwisho wa Malu kuimba. Alifariki dunia kwa kuanguka jukwaani akiwa anaimba wimbo huu, ambao aliurekodi akiwa na FM Academia miaka hiyo. Upo kwenye albamu ya 'Prison.'

### Binadamu

Huu ni wimbo maarufu sana, ulioitambulisha bendi ya Stono Musica, Malu akiwa mmoja wa waanzilishi pamoja na Ndanda Kosovo 'Kichaa.'


Bendi hii iliundwa baada ya kutokea mgawanyiko kwa wanamuziki wa FM Academia hasa baada ya kukubalika kwa wimbo wa 'Prison.'

Wale waliokwenda jela waliona kama wenzao wanapata umaarufu kupitia wao kutokana na bendi hiyo kuja na mtindo wa 'Wajelajela,' uliopendwa mno na mashabiki.

Walipoondoka wao wakajiita 'Wajelajela Original', na wimbo 'Binadamu', ukawatikisa mpaka FM Academia.

### Jimmy Chocolate

Ni moja kati ya nyimbo bora za Stono Musica, ambazo pia uliimbwa kwa ufundi mkubwa na Malu Stonch, Pacheco' na Ndanda.



FILAMU

# Tatoo: Penzi halisikiki, linaonekana

**Na Adam Fungamwango**

PENZI ni kitu cha ajabu sana, wazee wa zamani wanasema mwenye kupenda haoni wala hasikii.

Penzi ndiyo kitu pekee duniani kinachoweza kumtoa binadamu anayekaa Oysterbay au Masaki na kwenda kuishi Manzese, Tandale au Kigogo bila kuona tofauti yoyote ile.

Penzi la ukweli siku zote huonekana zaidi kuliko kusikika. Ukiiangalia na kuifuatilia filamu hii ya 'Tatoo' inaoyesha na kuthibitisha maneno haya.

Imechezwa na wasanii Elizabeth Michael, 'Lulu', Charles Magari, Hasnat Mathius, Mandela Nicholaus, Grace Mapunda na wengine wengi.

Inaanza kuonyesha kuwa Dastan, kijana wa kimasikini akimpenda Nicol, binti wa tajiri mzee Magari.

Alipokuja kugundua uhusiano huo, hakuupenda kutokana na tofauti hizo za kitabaka.

Kuna siku akawavizia, akawabamba, akawatoa mbio.

Anaporudi nyumbani, mzee Magari akampiga binti yake. Kwa hasira naye anakunywa sumu.

Habari zinamfikia Dastan, lakini hawezi kwenda msibani, badala yake baada ya mazishi anaamua kwenda kwenye kaburi la mpenzi wake.

Kwa bahati mbaya anakutwa na mzee Magari ambaye anampiga hadi kudondokea ukuta wa kaburi na kuzirai.

Madaktari wanashindwa kumtibia Dastan na kuamua kumpeleka kwenye wodi wa vichaa kwa uchunguzi zaidi.

Nyumbani kwa mzee Magari nako mambo sasa yanaanza kubadilika. Kijana wa wake Neron anamgeukia baba yake na kumwambia ukweli kuwa ana roho mbaya kwa sababu amesababisha kifo cha dada yake Nicol, naye akaoondoka nyumbani hapo ili akae kwenye nyumba yake ya kitajiri peke yake.

Naye anaamua kwenda kuishi na mpenzi wake ambaye ni masikini, Lulu. Huko Neron na mpenzi wake Lulu wanapanga mikakati ya kumuokoa Dastan kwenye hali yake ya kuchanganyikiwa.

Lulu anajichora tatoo inayofanana na ile aliyejichora marehemu Nicol wakati wa uhai wake. Halafu anajifanya kichaa ili apate nafasi ya kukutana na Dastan kwenye wodi yao.

Mpango huo unawahusisha pia madaktari ambao nao wanakula dili. Lulu anapachikwa hospitalini kwenye wodi ya vichaa, baada ya kujifanya kuwa amechanganyikiwa.

Baada ya kituko vya hapa na pale Lulu kumuonyesha Dastan tatoo kila wanapokutana, hatimaye kijana huyo anarejesha kumbukumbu nyuma na hatimaye fahamu zimamrudia. Akakumbuka kuwa alishawahi kumchora mpenzi wake tatoo kama hiyo miaka ya nyuma. Lulu alipoona Dastan, aliyekuwa mpenzi wa dada wa mpenzi wake Neron, akapanga kutoroka naye.

Mambo yalipokamilika, Lulu na Dastan walitoroka kutoka kwenye wodi ya vichaa.

Neron akiwa kwenye safari ya kumtembelea mapenzi wake Lulu na shemeji yake Dastan akiwa porini anamuona, msichana mmoja anakimbizwa na wahuni wakiwa na lengo la kumbaka. Neron anamsaidia lakini anapomuangalia sana msichana huyo haamini macho yake, kwani ni dada yake Nicol ambaye ilisemekana kuwa alifariki dunia na walishamzika.

Nicol anamwambia kaka yake kuwa hakufa, ila alipofika hospitalini alipatiwa matibabu na alipopata nafuu alitakiwa kueleza yote yaliyotokea na baada ya hapo, watu wa ustawi wa jamii walishauri akae mbali na familia yake kwanza, hivyo alipofika mzee Magari akaambiwa kuwa binti yake amefariki na akapewa maiti na msichana ambaye hakuwa na ndugu ili akazike.

Naron anamchukua dada yake na kumpeleka kwa mpenzi wake Dastan ambako pia Lulu yupo.

BONGO FLEVA

# Black Market Records kutafuta wasanii Tanzania




SOKO la muziki wa Bongo Fleva, linazidi kukua kwa kasi na kuwavutia wamiliki wa lebo mbalimbali duniani.

Hivi karibuni kiongozi Mkuu wa lebo ya Black Market Records ya nchini Marekani, Cedric Singleton, amefanya ziara nchini kwa ajili ya kuangalia namna ya kuwekeza katika muziki.

Tayari lebo hiyo imefanya vyema katika nchi mbili za Afrika Mashariki na kusababisha baadhi ya wasanii kupata mafanikio makubwa.

Akiwa jijini Dar es Salaam, Singleton, amesema kwamba lengo la ziara yake ni kuimarisha uhusiano na wadau mbalimbali ambao wamekuwa wakifanya nae kazi na kuwainua wasanii wake.

"Nimekuja Dar es Salaam kuangalia namna ya kuwainua wasanii, pia nitapita kwenye nchi nyingine za Afrika Mashariki kama Kenya na Uganda ambako huko kuna wasanii wanaosimamiwa na Black Market Records," amesema Singleton.

Black Market Records, imejizolea umaarufu mkubwa baada ya kuwa nyuma ya mafanikio ya wasanii wengi nchini Kenya na Uganda na Tanzania inatarajia kuingia katika orodha hiyo mwaka huu.

Kwa upande wa meneja wa Black Market Records nchini Kenya, Paulah BMR, amesema wamefanikiwa kufanya kazi na wasanii wakubwa kama vile Exray

Mbuzi Gang, Boondocks Gang, Daddy Andre, Nina Roz na Vic West.

## BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**Orchestre Sikinde Original**

Bendi hii inajiandaa kuingia studio kurekodi nyimbo za albamu ya kwanza ambapo itafanya onyesho moja tu la kesho Jumapili katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**FM Academia**

Wiki hii watakuwa na onyesho moja tu litakalofanyika kesho katika ukumbi wa Target Mbezi Beach.

**Twanga Pepeta**

Leo Jumamosi wapo Kiduli Garden Magomeni, kesho Jumapili watakuwa ndani ya ukumbi wa Gwambina Lounge Chang'ombe.

**Kimokimo Band**

Kama kawaida yao wakiwa chini ya mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa huwa ndani ya ukumbi wa Mariot uliopo eneo la Extertanal jijini Dar es Salaam.

**Mjengoni Classic Band**

Ikiwa nyumbani kwake jijini Arusha, leo Jumamosi itafanya makamuzi ndani ya ukumbi wa Kokoriko Annex, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wake wa nyumbani wa Mjengoni Club Orasiti jijini humo.

**Town Classic Band**

Leo Jumamosi watafanya vitu vyao ndani ya ukumbi wa Mawasiliano Ubungo, kesho wapo ndani ya ukumbi wa Twist Lounge Tabata.

**Waluguru Original**

Bendi hii yenye maskani yake mjini Morogoro, leo Jumamosi itatoa burudani ndani ya ukumbi wa Terminal Pub Msamvu, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wa F2 Florida mjini humo.

Tukuyu Sound Band

Kama kawaida yao, kila Jumapili vijana wa bendi hii watamalizia wikiendi yao katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park, uliopo Ubungo kando ya Barabara ya Sam Nujoma.



# Korra ashambuliwa kwa tindikali

MCHEZA dansi kutoka Nigeria, Anita Chukwumfumnaya Obidi, maarufu kama Korra Obidi, ameshambuliwa kwa visu na tindikali akiwa nchini Uingereza.

Shambulio hilo lilitokea wakati akiwa anaongea mubashara na mashabiki wake kupitia mtandao wa Instagram siku ya Alhamisi.

“Uso wangu unawaka, naomba msaada nijioshe tafadhali,” alisikika Obidi alisema huku akiugulia kwa maumivu.

Hata hivyo, watu waliofanya tukio hilo bado hawajakamatwa na katika video hiyo walionekana polisi wawili wakimsaidia kumpatia huduma ya kwanza.



## Msanii afa majini akiigiza

NOLLYWOOD imeingia katika hali ya majonzi kufuatia kifo cha muigizaji, Junior Pope, ambaye alizama majini wakati akicheza filamu.

Tukio hilo lilitokea Jumatano ya wiki hii wakati boti alilokuwa amepanda Pope kupinduka na yeye kuzama majini.

Kifo hicho kimesababisha vilio kutoka kwa watu mashuhuri, ambao walimlaumu mtayarishaji wa filamu hiyo kutokuwa makini katika kazi yake.

Mtayarishaji wa filamu hiyo inayoitwa The Other Side Of Life, anayeitwa Adamma Luke, amejikuta katika shinikizo kubwa akitakiwa kutoa maelezo ya kina sababu ya kutochukua hatua ya kiusalama wakati wa uchukuaji wa picha.

## Ja Rule aenda Ghana

RAPA mkongwe wa Marekani Ja Rule, ambaye jina lake halisi ni Jeffrey Bruce Atkins Sr, ametangaza kuelekea nchini Ghana kwa ajili ya kuanzisha mradi wa shule.

Mwimbaji huyo wa kibao cha ‘Mesmerize. Amesemna kupitia ukurasa wake wa Intagram kuwa atatembelea nchini humo kutoa huduma hiyo ya kielimu kwa watoto wasiokuwa na uwezo.

Mradi huu unatokana na mpango wa taasisi ya kimataifa ya Pencils Of Promise, inalenga kuleta elimu bora kwa watoto duniani kote





## J Cole ajutia kufanya hili...

RAPA na mtayarishaji wa muziki kutoka Marekani, J Cole ameomba radhi kwa mashabiki zake kutokana na kumuimba vibaya msanii mwenzake Kendrick Lamar.

Kupia ukurasa wake wa X, msanii huyo amesema amefanya kosa kubwa kumuimba vibaya Lamar kupitia wimbo wake wa “7 Minute Drill” unaopatikana kwenye Album yake mpya ya Might Delete Later.

J Cole amesema hajawahi kufanya jambo bayaka kama hilo katika maisha yake, hivyo ngoma hiyo ataitoa kwenye majukwaa yote ya muziki.

## Mnaomshangaa Umu Salma mnalo?

MWIGIZAJI na mjasiriamali wa nchini Nigeria, Umu Salma Mumin, amefunguka utajiri wake akisema unotokana na biashara na wanaume waliojitosheleza kifedha aliokuwa nao katika vipindi tofauti.

Katika mahojiano kwenye kipindi cha The Delay Show, staa huyo alifichua kuwa katika maisha yake amekuwa na bahati ya kuwa na wanaume wenye fedha, hivyo maisha yake hayawezi kuwa duni.

Amesema fedha zingine anapata kupitia biashara zake za nguo na vyakula anazofanya katika miji mikubwa nchini humo.



# Malalamiko waliohama Ngorongoro yamwibua DC

**Na Mwandishi Wetu,** HANDENI

MALALAMIKO ya baadhi ya wafugaji wa jamii ya Kimasai waliohama kwa hiari katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kwenda katika makazi mapya ya Msomera, wakidai kutotendewa haki, yamemwibua Mkuu wa Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, Albert Msando.

Msando alikutana jana na kufanya mazungumzo na wananchi hao wa kijiji cha Msomera kilichoko Kata ya Misima, huku akisisitiza serikali haitaruhusu mtu yeyote kufanya vitendo vya utapeli au udanganyifu katika mpango huo.

"Nimeamua kuja katika kijiji hiki ili kukutana na mwananchi yeyote ambaye anaamini kuwa serikali haijamtendea haki wakati wa kuhama kutoka ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kuja Msomera. Nimekuja kusikiliza malalamiko yenu na kutafuta suluhu ya kudumu kama yako madai ya msingi.

"Katika siku za hivi karibuni, kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya wananchi, ambao wakati wanahama kutoka Ngorongoro kuja Msomera, walikuwa wategemezi katika kaya mbalimbali, ambazo zilipwa stahiki zao zote za mali pamoja na motisha.

"Sasa wako waliojitokeza huko wakidai kuwa wametapeliwa na serikali kitu ambacho si cha kweli. Wananchi 132 ambao waliorodhesha majina yao na kuyaleta kwangu, niliyatuma majina hayo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro," alisema.

Katika kikao hicho, mkuu huyo wa wilaya alisema serikali imegundua kuwa watu hao hawakuwa wakuu wa kaya wakati wanahama.

"Kuna watu wanataka kuleta utapeli katika mpango huu na wengine wako nchi za nje, wakiamini kwamba kuna fedha za bure ili wafanye utapeli. Jambo hilo halikubaliki," alisema Msando. Kuhusu wananchi watatu ambao majina yao yameongezeka katika taarifa iliyotolewa na baadhi ya vyombo vya habari, Msando alisema vyombo husika vinafuatilia madai yao kuona kama yana ukweli.

Wananchi 132 ambao ni wategemezi wa kaya zilizohama kwa hiyari kutoka ndani ya hifadhi ya Ngorongoro kwenda Msomera, waliripotiwa na baadhi ya vyombo vya habari kwamba serikali haijawapa stahiki zao wakati wa zoezi hilo la kuhama.

Awamu ya kwanza, serikali ilijenga nyumba 503 katika kijiji cha Msomera na kuwezesha kaya 551 kuhamia zikiwa na watu 3,010 na mifugo 15,521.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mohamed Mfaki (kushoto), akizungumza na vijana waliokuwa wakisheherekea siku yao ya kuzaliwa, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti, iliyobeba ujumbe unaosema "Panda Mti Siku ya Kuzaliwa, Kata Keki Panda Mti" katika ofisi ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), wilayani humo, juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Hatimaye wajengewa zahanati tangu uhuru

**Na Mwandishi Wetu,** MWANGA

WANANCHI 955 wa kijiji cha Kwanyange, Mwanga mkoani Kilimanjaro, waliokuwa hawana huduma za afya karibu na makazi yao tangu nchi ilipopata uhuru, sasa wameondokana na adha hiyo baada ya kuanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho.

Kwanyange ni miongoni mwa vijiji vya pembezoni ambavyo vimekuwa vikishuhudia baadhi ya wanawake wajawazito wakipoteza maisha kutokana na kushindwa kufikia huduma za afya.

Mkuu wa Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Wilaya hiyo, Dk. Serijo Kusekwa, alisema jana kuwa zahanati hiyo itakuwa mkombozi kwa wananchi hao ambao walikuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma za afya hasa za baba, mama na mtoto pamoja na ushauri nasihi.

"Ni kweli wananchi hawa walikuwa wanapata shida kufikia huduma za afya, walisafiri umbali mrefu na kutumia fedha nyingi kufuata huduma Hospitali ya Wilaya ya Mwanga, lakini hivi sasa serikali imeamua kuwasogezea hiyo huduma kijijini kwao.

"Mradi wa ujenzi wa Zahanati hiyo, unatekekezwa kwa utaratibu wa force account (mafundi jamii). Kazi zinazoendelea ni kuweka sakafu, kupaka rangi, kujenga kichomea taka, shimo la kondo la nyuma na kuweka madirisha pamoja na milango," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Kusekwa, mradi huo utaigharimu serikali zaidi ya Sh. milioni 164.101.

Katika mradi huo, Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga imechangia Sh. 38,135,407, Mfuko wa Jimbo, Sh. milioni 1.6, serikali kuu Sh. milioni 50 na nguvu za wananchi Sh. 900,000.

Mmoja wa wananchi waliozungumza na Nipashe, Mariam Rashid, alisema wanayo matumaini makubwa kuwa zahanati hiyo itawasaidia kupunguza vifo vya wajawazito waliokuwa wakipoteza maisha njiani, wakati wanakwenda kujifungua pamoja na watoto wachanga.

## Wapata mwarobaini wabadiliko tabianchi

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

VIJIJI 10 vinavyokaliwa na jamii za kifugaji katika Wilaya za Longido na Ngorongoro mkoani Arusha, ambavyo baadhi ya maeneo yake yanatishiwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, wamepata 'mwarobaini' unaohimili tatizo hilo.

Ili kukabilina na hali hiyo, wameanza kuutumia mradi jumuishi wa mazingira na kuboresha maisha ya jamii, utakaosadia kurejesha uoto wa asili na vyanzo vya maji unaofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhifadhi na Mazingira (IUCN).

Ofisa Programu wa IUCN, Ng'walu Kidayi, jana alisema kuwa mradi huo, pia utapita kwenye maeneo ya Ziwa Natron, Ziwa Eyasi na Bonde la Yaeda, linalokaliwa na makabila ya Wadatoga na jamii ya wawindaji, waokota matunda na warina asali ya Hadzabe.

Akizungumzia mradi huo ambao utashirikisha wananchi katika shughuli zote zinazohusu uhifadhi endelevu, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marko Ng'umbi alisema:

"Kwa bahati nzuri wilaya hii ina vijiji 49 na vyote vina ramani na vimepimwa," alisema.

Mratibu wa UCRT wa Wilaya ya Longido, Jamboi Baramayesu, alisema mradi huo unagharimu dola za Marekani milioni 1.488, sawa na zaidi ya Sh. bilioni tatu.

Kwa mujibu wa Baramayesu, mradi huo unatarajia kuvinufaisha vijiji 10 vya Wilaya za Longido na Ngorongoro.

"Mradi huu unahudumia klasta tatu, ambazo ni klasta ya Ziwa Natron na Longido Magharibi, na klasta ya pili ni ya Ziwa Eyasi na Bonde la Yaeda, wakati ya tatu ni Simanjiro na Kiteto.

Kwa klasta ya Ziwa Natron na Longido Magharibi, vijiji vinavyopitiwa na mradi ni 10, kwa maana ya Ngorongoro vinne na Longido, vijiji sita," alisema.

Naye Richard Mollel alisema mradi huo ni rafiki kwao, na ni moja ya aina ya mradi unaotakiwa katika jamii ya kifugaji kutokana na kuwa shirikishi na unaojumuisha binadamu na wanyama.

Mkazi mwingine, Hellena John, alisema mradi huo unawapa fursa ya kushiriki katika kuhifadhi vyanzo vya maji, ambavyo vimekuwa vikivamiwa kwa namna moja ama nyingine kutokana na kutokuwepo kwa mipaka thabiti.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Sam Mangwana, Mkongo aliyeishi Manzese, anayeongea kiswahili kama Mbongo tu

## -Akapaisha washkaji zake, Anania, Kamanga






**Na Adam Fungamwango**

MARA ya kwanza tulipoonana alinisalimia. Aliambia ananitambua kutokana na mapicha yangu. Mwanamke mzuri kama malaika, anavyotembea ni kama nguva ndani ya bahari. Tafadhali nielezee kwenu wapi. Akasema anatoka Afrika ya Mashariki, nyumbani kwao Tanga. Usiumize Kabibi. Anania wangu yuko Dar. Sikia tabu niliyopata. Kamanga wangu Manzese."

Ni baadhi ya mashairi yaliyomo kwenye wimbo wa mwanamuziki maarufu barani Afrika, Sam Mangwana, uliotoka mwanzoni mwa miaka ya 1980, uitwao 'Kabibi.'

Katika wimbo huo anawata

Mwanamuziki ambaye pamoja na kuwa ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, aliuimba kwa kiswahili kizuri sana.

Hapo kuna maneno anasema Anania wake yupo Dar, na Kamanga wake Manzese.

Kuna mashabiki wengi wa muziki wanapata tabu sana wakisikia maneno hayo na hawajui kwa nini Mangwana aliimba hivyo. Hao ni marafiki zake, washkaji au wafadhili wake, ambao humpa kampani kila anapokuja nchini Tanzania.

Ambalo mashabiki wengi wa Bongo hawajui ni kwamba huyu jamaa aliishi kwa muda fulani Tanzania, hasa jijini Dar es Salaam mwanzoni kabisa mwa miaka ya 1980.

Akiwa nchini alikuwa anaishi maeneo ya Manzese Midizini kwa rafiki yake huyo Kamanga. Na hata kila alipokuwa akija nchini alifikia hapo hata akirudi leo, Mangwana humpotezi mitaa ya Manzese, anaijua vilivyo. Labda tu anaweza kushangaa kwa jinsi ilivyojengeka tofauti na alivyoondoka.

Hebu tuwafahamu marafiki hao wa Mangwana aliowaimba kwenye wimbo wa 'Kabibi' ni kina nani

Kamanga alikuwa mmoja wa wafanyabiashara maarufu nchini, na mwingine alikuwa ni Anania Sangula aliyewahi kuwa mcheza soka kwenye klabu ya Simba miaka ya 1970, kabla ya kuwa mfanyakazi kwenye kiwanda cha bia wakati huo.

Kutokana na urafiki wao mkubwa na ukarimu wa hali ya juu waliokuwa wakimfanyia kila alipokuwa akija mchini, akawatunuku kwa kuwataja kwenye wimbo wa 'Kabibi.'

Pia si wengi wanaojua kuwa alishawahi kupigia bendi za Maquiz du Zaire na Vijana Jazz Band.

Nyimbo za 'Mary Maria', 'Tambiko la Pambamoto', na 'Bujumbura' ambazo zilitungwa na hayati Hemed Maneti, kwa kiasi kikubwa zilichangiwa na Mangwana kwenye utengenezaji wake hadi zikakaa sawa.

Ndiyo maana ukichunguza nyimbo hizo, uimbaji wake na upigaji, ni tofauti na nyimbo za Vijana Jazz zilizopita kabla ya albamu hiyo.

Umaarufu wa Mangwana ulianza tangu mwanzoni mwa 1970, na ukitaka kujua kuwa ni mwanamuziki mkubwa amezipigia bendi zote kubwa nchini DR Coango, za TP OK Jazz chini ya hayati Luambo Luanzo Makiadi Franco, na Afrisa International, chini ya hayati Tabu Ley Rochereau. Hadi leo yupo hai na anaendelea na muziki.

Huyu jamaa ni Mkongomani aliyezaliwa jijini Kinshasa, mji mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ingawa wazazi wake hawakuwa Wakongomani. Baba yake alikuwa ni Mzimbabwe na mama yake alikuwa raia wa Angola.

Ni mmoja wa wanamuziki wachache wanaojua lugha nyingi mno. Akiimba Kiswahili unaweza ukadhani amezaliwa Dar.

Tatizo la Mangwana ni mwanamuziki asiyetulia. Huwa hakai bendi moja. Alikaa muda mfupi kwenye bendi zote mbili kama mwanamuziki mualikwa na akaondoka zake nchini Kenya, akakaa kidogo, akaenda zake Ulaya na kwa sasa anafanya shughuli zake kwenye nchi za Ufaransa na Ubelgiji.

**Tuma meseji 0716 350534**



# Serikali Mali yageukia waandishi wa habari

**BAMAKO,** MALI

SERIKALI ya kijeshi nchini Mali, imepiga marufuku vyombo vya habari kuripoti shughuli za vyama na makundi ya kisiasa.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya siku moja serikali hiyo kusimamisha shughuli zote za kisiasa kwa muda usiojulikana katika nchi hiyo.

Tangazo hilo lilitolewa juzi na uongozi wa mamlaka ya mawasiliano na kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii. Taarifa hiyo ilitaka vyombo vyote vya habari ikiwemo vituo vya redio,Televisheni, mtandao na magazeti vinahusika na utekelezaji wake.

Hata hivyo, haikufafanuliwa kwa kina ni kwa namna gani ufuatiliaji wa hatua ya marufuku hiyo utatekelezwa.

Shirika linalowawakilisha waandishi habari nchini Mali, limeipinga hatua hiyo ya serikali na kuwatolea wito waandishi waendelee kuripoti kuhusu masuala ya kisiasa na kusimama imara kutetea haki ya mwananchi ya kupata habari.

Mali imekumbwa na mapinduzi mara mbili tangu mwaka 2020, yaliyosababisha hali mbaya ya uthabiti wa kisiasa ambayo imeshuhudiwa pia katika mataifa mengine ya Afrika Magharibi na Kati kuingia katika mapinduzi.

**DW**

# Polisi Ethiopia wapambana na waasi

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

POLISI nchini Ethiopia imewaua watu watatu baada ya kutokea tukio la ufyatulianaji risasi katika mji mkuu wa Addis Ababa.

Kulingana na taarifa ya polisi ilieleza waliouawa mmoja alikuwa raia, waliobaki wanaodaiwa kuwa wanamgambo wa kundi la waasi la Fano.

Katika tukio hilo lililotokea jana asubuhi katika mtaa wa watu matajiri, polisi wawili walijeruhiwa.

Kundi la Fano linafanya kazi katika jimbo la Amhara ambalo limekuwa likipambana na jeshi tangu Agosti mwaka jana.

# Marekani yatahadharisha Iran kuishambulia Israel

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imezuia kusafiri kwa maofisa wake wa ubalozi wanaofanya kazi nchini Israel kutokana na hofu nchi hiyo kushambuliwa na Iran.

Taarifa kutoka ubalozi wa Marekani nchini humo, ulisema wafanyakazi wameambiwa wasisafiri nje ya miji mikubwa ya Jerusalem, Tel Aviv au Beersheba kutokana na tahadhari nyingi za kushambuliwa.

Nchi ya Iran imeapa kulipiza kisasi, ikiilaumu Israel kwa kushambulia ubalozi wake mdogo nchini Syria siku 11 zilizopita na kuua watu 13.

Wakati huo huo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, Lord Cameron, amempigia simu waziri mwenzake wa Iran kuhimiza kupunguza kuongezeka kwa mzozo huo.

Israel kwa upande wake haijakiri kuhusika na shambulizi hilo la ubalozi mdogo, lakini inachukuliwa kuwa ndiyo muhusika mkuu.

Nchi ya Iran inaunga mkono kundi la Hamas linaloongoza Ukanda wa Gaza pamoja na makundi mbalimbali yaliyo katika eneo hilo likiwamo Hezbollah la nchini Lebanon ambalo mara kwa mara hufanya mashambulizi dhidi ya Waisraeli. Waliouawa katika shambulio hilo la ubalozi mdogo ni pamoja na kamanda mkuu wa kikosi cha wasomi cha Iran cha Quds katika nchi za Syria na Lebanon.

Shambulio hilo limetokea wakati wa juhudi za kidiplomasia zinazofanyika kuzuia vita vya Gaza kuenea katika eneo hilo.

Akizungumza hivi karibuni, Rais wa Marekani, Joe Biden, aliionya Iran kuwa inatishia kufanya shambulio kubwa nchini Israel na aliapa kutoa msaada kwa taifa hilo.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alisema serikali yake iko tayari kukabiliana na changamoto yoyote ya kiusalama, akionya kuwa Israel itaidhuru nchi yoyote itakayoiletea madhara.


Wakati huo huo, waandamanaji walimiminika katika viunga vya mji mkuu wa Israel, Tel Aviv, kuikosoa serikali ya Netanyahu na kutoa wito wa kuachiwa huru mateka wanaoshikiliwa na Hamas, Gaza.

Wengi wa waandamanaji walikuwa wamebeba mabango yenye picha za mateka ambao inaaminika bado wanashikiliwa na kundi la Hamas ndani ya Ukanda wa Gaza tangu walipotekwa nyara Oktoba 7 mwaka jana.

Maandamano hayo yanafuatia mengine makubwa yaliyofanyika mwanzoni mwa mwezi huu mjini Jerusalem katika kile kinachoonekana kuwepo kwa mgawanyiko miongoni mwa raia wa Israeli, hasa kuhusu namna Netanyahu anavyoushughulikia mzozo huo.

Tayari shinikizo linaongezeka la kutaka kuitishwe uchaguzi wa mapema, lakini Netanyahu amesema utavuruga kampeni yake dhidi ya Hamas na kukwamisha mazungumzo ya kuachiwa kwa mateka.

**BBC**



Rais wa Somalia Hassan Sheikh Mohamud akifanya mazungumzo na Rais wa Kenya, William Ruto, katika ziara yake aliyoifanya nchini humo katika juhudi za kutafuta suluhu ya mgogoro kati ya nchi yake na Ethiopia. **PICHA: REUTERS**

# Russia kuendelea kuipiga mifumo ya ulinzi Ukraine

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vradimir Putin, amesema mashambulizi dhidi ya mtambo wa nishati nchini Ukraine ni muhimu kufanyika ili kuondoa ulinzi wa kijeshi.

Akizungumzia suala hilo, Putin alisema kwamba nchi yake ilijizuia kufanya mashambulizi ya aina hiyo wakati wa majira ya baridi, lakini sasa yanahitajika kwa ajili ya kumaliza vita.

"Kwa sababu za kibinadamu, hatukufanya shambulio lolote wakati wa msimu wa baridi, tukikumbuka kwamba hatukutaka kuacha taasisi za kijamii, hospitali, na kadhalika bila usambazaji wa umeme. Lakini baada ya mashambulizi kwenye vituo vyetu vya nishati, tulilazimika kujibu," alisema Rais Putin. Kauli hiyo aliitoa wakati wa mkutano na mshirika wake Rais wa Belarus, Alexander Lukashenko.

Rais Putin alitaja lengo lingine ambalo pia alilitangaza katika hotuba yake ya Februari 24, mwaka huu ni kuondoa utawala wa kinazi.

Wakati sekta ya nishati ikilengwa, pia Rais Putin alisema mifumo ya ulinzi ni moja ya shabaha ya mashambulizi.

"Kwa bahati mbaya, tumeona mfululizo wa mashambulizi kwenye vituo vyetu vya nishati hivi karibuni na imebidi kujibu.",alisisitiza kiongozi huyo.

Ukraine hivi karibuni ilishambulia vituo vya kusafisha mafuta vya Russia na vifaa vya kuhifadhi mafuta na kusababisha upungufu wa uzalishaji wa petroli nchini humo.

Katika kujibu mapigo, Russia ilishambulia sekta ya nishati ya Ukraine katika msimu wa majira ya joto na msimu wa baridi mwaka huu.

Rais Putin, pia alieleza uvamizi wa mitambo ya kuzalisha umeme mwaka wa 2022 kuwa hatua ya kulipiza kisasi, na pia kujibu uharibifu wa daraja katika Mlango-Bahari wa Kerch.

Alisema matukio mengi ya kushambulia ni hatua ya kulipiza kisasi ya kulazimishwa.

**BBC**

# MATUKIO KATIKA PICHA



Rais Samia Suluhu Hassan akiteta jambo na Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mwadhama Kardinali Polycarp Pengo baada ya Ibada ya Misa Takatifu ya Kumbukizi ya miaka 40 tangu kutokea kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward Moringe Sokoine, wilayani Monduli mkoani Arusha jana. **PICHA: IKULU**



Baadhi ya nyumba za eneo la Malamba Mawili, Dar es Salaam, zikiwa hatarini kubomoka baada ya kutokea kwa mmomonyoko mkubwa wa ardhi, unaosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha, kama ilivyonaswa na kamera yetu jana. **PICHA: SABATO KASIKA**



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mbunge wa Muheza, Hamisi Mwinjuma ‘Mwana FA’ (kulia), akisalimiana na Mkuu wa wilaya ya Muheza, Zainabu Abdallah alipowasili kwa ajili ya kongamano la vijana wilayani humo jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Rais wa Zanzibar, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Wananchi wa Kijiji cha Kilimani Tazari Kidoti, baada ya kumalizika kwa ibada ya swala ya Ijumaa katika Masjid Hidaya Kilimani Tazari Zanzibar jana. PICHA: IKULU **PICHA: OSCAR ASSENGA**



Shekhe Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zubeir akizungumza baada ya swala ya Ijumaa katika Msikiti Mkuu wa Mfalme Mohammed VI wa Morocco, Kinondoni Dar es Salaaam jana, akiwataka mashekhe wa mikoa , wilaya na maimamu nchini kumuomba Mungu aepushe athari mbaya zinazotokana na mvua zinazoendelea kunyesha. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Vyombo vya usafiri vikipita kwa tabu katika shimo kubwa lililotuama maji kutokana na mvua za masika zilizoanza kunyesha katika eneo la Kitunda Kati, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-8

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Mwingine aliyekuwa na wasiwasi ni Kamal. Mpenzi wa Mariamu. Mara ya mwisho inasemekana aliongea na mpenzi wake ambaye alimwambia anakata atoke nyumbani ili akakague na kufunga biashara zake.

Baada ya nusu baadaye simu ilikuwa haipatikani. Haikupatikana kwa muda mrefu ambapo si kawaida yake.

Akaamua kwenda nyumbani wake. Kamal na Mariamu pamoja na kwamba ni wapenzi, lakini kila mmoja bado anaishi kivyake, bado hawakuwa wameanza kukaa pamoja.

Kamal akaamua kumfuata Mariamu na bodaboda hadi nyumbani kwake. Ilikuwa ni saa sita usiku. Akagonga lakini wapi. Simu nayo haipatikani. Kitu cha kwanza alichofanya ni kuamua kufungua mlango na kuingia ndani. Kamal alikuwa na funguo zote za nyumba anayoishi mpenzi wake.

Alipoingia ndani aliona dalili zote za Mariamu kuondoka hapo. Pamoja na kwamba anamuamini sana, lakini akaanza kuwa na wasiwasi kuwa anazoziona sasa ni dalili za usaliti.

Hata hivyo, katika pekuapukua aliikuta simu ya Mariamu ndani. Ni kama alikuwa ameisahau hivi kwa sababu ilikuwa mezani. Akili yake ikamtuma kuwa alikuwa ameisahau na si vinginevyo.

Hata hivyo kilichomshtua ni kwa nini hajarudi kuichukua? Vyovyote iwavyo, isingewezekana mtu aliyesahau simu akakaa zaidi ya masaa manne hajarejea kuifuata. Hii ikazidi kumtia wasiwasi kuwa huenda yupo kwenye matatizo zaidi, na si kama anavyodhani kuwa amekwenda kwa bwana.


***********************************

"Tuna wasiwasi kubwa kifo cha ndugu yetu siyo kama tulivyoelezwa mwanzo. Tuna wasiwasi kuna kitu kingine zaidi ya hiki." Ni baba mdogo wa marehemu Mariamu Salumu. Yeye ndiye aliteuliwa kama msemaji wa familia. Alikuwa akiongea mbele ya waandishi wa habari.

Ni baada ya ripoti ya madaktari kutoka. Baada ya kumpima marehemu ilionekana alifariki kwa ugonjwa wa shinikizo la damu wakati akifanya mazoezi maeneo ya Tabata.

Taarifa ya madaktari inasema baada ya kupatwa na presha ya ghafla ilimfanya sishiwe nguvu apepesuke na kuanguka ndani ya mtaro ulio pembezoni mwa barabara.

"Ripoti inasema alipatwa na presha ndiyo akaanguka ndani ya mtaro, kwa hiyo ndiyo iliyomuua wanavyosema, lakini maiti ya tuliikuta na jereha kama mtu aliyechomwa au kupigwa na kitu kizito kichwani. Tumeuliza, wakatuambia hiyo imetokana na kuangua. Jinsi alivyoanguka, inaonekana kuna kitu ameangukia kwa sababu kuna uwezekano mkubwa mtu anayeanguka akapata jeraha kichwani," akasema Timo Paul baba yake mdogo marehemu Mariamu.




**Ujumbe huu ulionekana kuwagusa waandishi wa kutaka kujua ni kitu gani ambacho kitafanyika kama ikionekana aliuawa.**

"Sawa sisi tunakubali hiyo inaweza kutokea, lakini wasiwasi wetu sisi ni kwamba ndugu yetu ameuawa." Akasema na kuwaangalia Waandishi wa Habari ambao walikuwa wamenyoosha vidole kutaka kumuuliza maswali.

Alipoulizwa kwa nini anaamini hivyo, akawaambia simu yake haikupatikana tangu usiku kuamkia alfajiri ambayo aliokotwa kwenye mtaro.

"Usiku, tena siyo wa manane, saa 2:00 tu usiku simu ilikuwa haiiti. Ina maana alikuwa matatizoni tangu wakati huo, na si kweli alianguka wakati akiwa mazoezini.

Niwaambieni nyinyi waandishi, hivi mtu tangu usiku saa mbili simu haipatikani, hadi kesho yake asubuhi ndiyo akutwe amekufa kweli?

Na pia niwaambieni tu simu yake imekutwa ndani wake. Hakuichukua, labda kwa makusudi au aliisahau. Au alikuja kutekwa ndani. Unajua watekaji hawawezi kuchukua wakakwambia uchukue na simu yako.

Kwa maana hiyo wanaweza kuwa wameingia wakamchukua wakaenda kumuua na kwenda kumtupa kwenye mtaro, sisi ndugu tunaamini hivyo." Akaongea kwa sauti na uchungu.

Waandishi waliendelea kumuuliza maswali ambayo yaliendelea kumfanya kufunguka kwa kile yeye na familia yake waliamini kutokana na mazingira waliyoyaona.

"Kuna kijana mmoja ambaye mchumba wake, na juzi tu ameleta barua ya posa, ametuambia mara ya mwisho walivyowasiliana alimwambia anataka kutoa nyumbani kwenda kukagua na kufunga biashara zake, lakini nusu saa baadaye simu yake ilikuwa haipatikani, akamfuata mpaka kwake, si unajua tena vijana wivu. Akamfuata nyumbani, kufika akakuta mlango umefungwa, kwa sababu ana ufunguo wake akafungua alipoingia hakumkuta kweli, lakini akakuta simu ikiwa imezimwa iko kwenye chaji. Hii inaonyesha kuwa marehemu hakutoka ndani humo kwa hiari yake."

Baada ya maelezo ya dhana mbalimbali kuhusu kifo cha Mariamu, Waandishi wakamuuliza uamuzi ambao familia imechukua au itachukua.

"Tunaamini kuwa taarifa aliyopewa Kamanda haikuwa sahihi kwa asilimia zote. Zingine ni sahihi, lakini ukweli ni kwamba ndugu yetu hakuanguka akiwa kwenye mazoezi. Tunajua ni kweli alikuwa anafanya mazoezi ya jogging, lakini hakuwa na rekodi yoyote ya ugonjwa wa moyo. Pia mchumba wake amesema ana wasiwasi kwa sababu hata nguo alizokutwa nazo alikuwa hajawahi kuziona hata siku moja amevaa. Zile sare za mazoezi machoni mwake ni mpya, na akatuambia sare zake zote alizikuta ndani, lakini hizo alizokuwa amekutwa nazo amefariki zilikuwa mpya, labda alikuwa amezinunua siku moja au mbili zilizopita kwa sababu wapenzi hawa hawakai wote bado, kila mtu akasihi kwake, wanatembeleana tu."

Alinyanyua chupa yake ya maji, akapiga mafunda kadhaa, auirudisha mezani.

"Tunaliomba Jeshi la Polisi lifanye tena uchunguzi wa kina, kuna kitu hapa katikati, ndugu yetu amedhulumiwa nafasi," alisema na akaingiza kwenye mfumo wa shati na kutoa karatasi.

"Hapa nina ujumbe kutoka kwa wazee wa familia. wamenipa ujumbe huu uwafikie. Wanasema kama ndugu yao amekufa kifo cha kawaida kama kinavyoelezwa ameanguka kwa presha na kufa sawa, lakini kama kuna mkono wa mtu basi hawatokubali kamwe."

Ujumbe huu ulionekana kuwagusa waandishi wa kutaka kujua ni kitu gani ambacho kitafanyika kama ikionekana aliuawa.

"Wamesema vyovyote itakavyokuwa, kama ameuawa, basi damu ya marehemu haitoenda bure. Damu ya Mariamu itawalilia wote waliomuua. Damu ya Mariamu haitokauka ardhini. Damu ya Mariamu itaendelea kumiminika kama chemchem, mpaka pale wote waliohusika wanapatikana na kupata kinachowastahili.

Wazee wamesema wao hawatomaliza msiba huu mpaka wale wote waliofanya hivyo wafahamike na kupata adhabu yao hapa hapa duniani. Hapo ndipo watamaliza msiba, na watajua kuwa ndugu yao sasa amefurahi na kulala kwa amani. Nadhani Jeshi la Polisi ambalo lina nia ya dhati kwa wananchi wake litafanya kama tulivyoagiza. Vinginevyo familia itamshtakia Mungu.

**Itaendelea Jumamosi**

# JULIO 'AIKIMBIA' SINGIDA FG FC AKILIA KUBORESHWA MKATABA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Jamhuri Kihwelo (Julio) amesema amerejea Dar es Salaam kwa lengo la kuweka sawa hatima ya mkataba wake wa kuifundisha timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Julio amesema hayo baada ya kutokea sintofahamu katika nafasi yake na kuamua kuiacha kwa muda timu hiyo inayokabiliwa na mchezo 'mgumu' dhidi ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Julio alisema hajafukuzwa wala kuondolewa na kiongozi yoyote ndani ya timu hiyo bali amefikia uamuzi huo kwa ajili ya kukutana na bosi wake havikuwa sawa sawa na amelazimika kurekebisha mapema kabla mambo hayajaharibika.

Julio alisema kuna baadhi ya vipengele katika mkataba wake havikuwa sawa sawa na amelazimika kurekebisha mapema kabla mambo hayajaharibika.

Alisema kipindi yupo nje ya timu hiyo ameiacha ikiwa salama baada ya kuandaa kikosi chake kwa ajili ya kuwakaribisha Yanga na kwa sasa kikosi kitakuwa chini ya Kocha Msaidizi, Ngawina Ngawina.

"Nimeandaa timu na ipo chini ya kocha Ngawina, nimekuja kukutana na bosi ili kuweka sawa mkataba wangu katika kutekeleza majukumu, tutakutana kumaliza hili na tukienda sawa nitarejea kuendelea nilipoishia.

Kuna vitu tulivyokubalia havijakaa sawa, nimeamua kuja kuyajenga na bosi, kwa sababu makocha wazawa hatupewi thamani tofauti na wenzetu wa kigeni hukamilishiwa mahitaji yao mapema kabla ya kuanza kazi," Julio alisema.

Kocha huyo aliongeza anaimani mambo yatakwenda sawa huku akiwaambia mashabiki wa Singida Fountain Gate FC timu yao haitashuka daraja na itaendelea kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi.

"Haitashuka daraja kwa sababu ninatarajia kuweka sawa mambo ambayo yatatupeleka katika kufikia malengo ikiwamo kuandaa timu vizuri, kuzungumza na wachezaji lakini kuweka mipango itakayohakikisha tunafanikiwa kupata alama katika michezo nane iliyosalia," aliongeza kocha huyo wa zamani wa Simba na Namungo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Singida Fountain Gate iko katika nafasi ya saba ikiwa na pointi 24 wakati timu inayoburuza mkia ni Mtibwa Sugar yenye 16.

Yanga yenye pointi 52 ndio mabingwa watetezi na vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na Azam FC yenye pointi 47 na Simba ikiwa kwenye nafasi ya tatu na pointi zake 45 kibindoni, lakini imecheza michezo pungufu ukilinganisha na walioko juu yake.



Wachezaji wa Ihefu sasa inajulikana kama Singida Black Stars wakifanya mazoezi kujiandaa kuikaribisha Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani, Singida. **PICHA: MTANDAO**

# Mtibwa yawaza pointi 12 Bara

**Na Saada Akida**

WAKATI wakiwa na kibarua cha ugenini dhidi ya Geita Gold FC leo, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema mipango ya kikosi chake ni kupambana kuvuna pointi 12 za michezo minne ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayofuata.

Katwila alisema endapo watashinda mechi nne zinazokuja, malengo yao ya kujiondoa katika hatari ya kushuka daraja yataondoka na hatimaye kujiweka mahali salama.

Kocha huyo alisema nafasi waliyopo katika msimamo wa ligi hiyo ni mbaya na watalazimika kupambana kubadilisha 'upepo' na hatimaye kupata matokeo chanya yatakayowasalimisha kwenye mbio zao.

Alisema wanatambua wako katika kipindi kigumu na wachezaji wake watacheza kwa presha ili kuhakikisha 'ndoto' za kubakia katika ligi hiyo zinatimia.

"Ni kweli tuko katika nafasi mbaya, lakini tunaweza kujiondoa kwenye nafasi hii kwa kupata pointi katika kila mechi iliyopo mbele yetu, nimewaandaa wachezaji wangu kiakili na kimbinu, pia kutocheza kwa presha kubwa," aliongeza Katwila.

Kiungo huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar alisema endapo watacheza bila presha, ana uhakika watapata ushindi na kujiondoa kwenye janga hilo ambalo linawazunguka.

"Ninataka kuvuna pointi 12 katika mechi zetu nne zinazokuja, hizi mechi ndio zitatupa picha ya hatima yetu," aliongeza kocha huyo.

## Kadio, Nyenza wapeta gofu kumwenzi Lina

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

WACHEZAJI wa kulipwa wa gofu kutoka Dar es Salaam, Bryson Nyenza na Hassan Kadio, wameibuka vinara wa raundi 18 za kwanza za mashindano maalumu ya gofu ya kumwenzi mchezaji wa zamani wa timu ya wanawake, Lina Nkya, baada ya kuongoza kwa mkwaju mmoja.

Nyenza na Kadio walimaliza raundi 18 za awali kwa mikwaju 73, kila mmoja, yaani mkwaju mmoja zaidi ya mshindi wa pili, Nuru Mollel, aliyepiga mikwaju 74.

"Mchezo bado ni mgumu ingawa nimeweza kuongoza siku ya ufunguzi kwa sababu bado kuna raundi nyingine 54 mbele yetu," alisema Nyenza.

Licha ya kuwa nyuma kwa mkwaju mmoja, Mollel, bado ana imani ya kufanya vizuri katika raundi tatu zilizobaki ili kumaliza mashimo 54 yaliyobaki.

**"Nina uzoefu wa kutosha na fimbo mmoja si kitu kikubwa, nafikiri nitakuwa vizuri zaidi katika mashimo 54 yaliyobaki," alisema Mollel.**

Mambo hayakuwa mazuri kwa Angel Eaton, mchezaji wa kike pekee wa kulipwa katika mashindano hayo baada kupiga mikwaju 84.

"Matokeo ya leo (juzi), si mazuri kwangu, lakini naweza kupata matokeo mazuri zaidi katika raundi zinazofuata. Nitapambana hadi kushinda azma hii," alisema Eaton.

Lina GP Tour ni mfululizo wa michuano ya gofu mahususi kwa ajili ya kumwenzi, Lina Said Nkya, ambaye alikuwa Mama Mlezi wa gofu kwa Wanawake Tanzania, enzi za uhai wake.

Mashindano haya yanayojumuisha wachezaji gofu wa ridhaa na kulipwa ambao wako katika orodha ya viwango vya Pro-Am yatachezwa katika viwanja vitano.

"Familia ya wanagofu ilineemeka sana na Lina Nkya kwa sababu mchango wake haujulikani ndio maana yameanzishwa mashindano hayo," alisema Ayne Magombe, mmoja wa wachezaji wa timu ya taifa ya gofu ya wanawake nchini.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MUSIALA ANUKIA CITY**
KLABU ya Manchester City inaongoza kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Bayern Munich Mjerumani, Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 21 lakini Liverpool, Barcelona na Paris St-Germain zote zinamtaka nyota huyo. (***Independent***)

**TONEY KUTUA UNITED**
BRENTFORD inatarajia mshambuliaji wa England, Ivan Toney kuondoka katika klabu hiyo msimu wa joto, lakini Nyuki hao watataka pauni milioni 50, huku Manchester United wakiwa miongoni mwa timu za Ligi Kuu England zikimfuatilia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.(***HITC***)

**ASHWORTH AKARIBIA UNITED**
SIR Jim Ratcliffe amefanya mazungumzo ya ana kwa ana na mmiliki wa Newcastle United, Amanda Staveley katika kujaribu kufikia makubaliano juu ya uhamisho wa mkurugenzi wa michezo, Dan Ashworth kwenda Manchester United.(***Times***)

**HAVERTZ MAMBO SAFI**
HALI nzuri ya mchezo wa fowadi wa Arsenal, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 24 imewafanya washikabunduki kufikiria upya mipango yao ya uhamisho wa majira ya joto.(***Mirror***)

**VARANE KUONDOKA UNITED**
MCHEZAJI Mfaransa Raphael Varane mwenye umri wa miaka 30, hatapewa mkataba mpya na Manchester United na anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo mkataba wake wa sasa utakapokamilika Juni, mwaka huu.(***Chris Wheeler, Mail***)

**PATINO KUONDOKA ENGLAND**
KIUNGO wa kati wa Arsenal, Charlie Patino mwenye umri wa miaka 20, yuko tayari kwa uhamisho wa majira ya joto nje ya England.(***Evening Standard***)

**AMORIM, LIVERPOOL SAFI**
KLABU ya Liverpool imeripotiwa kwamba imefikia mekubaliana na kocha wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim. (***Football Insider***)

**HINCAPIE ANUKIA SPURS**
KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou ameka kipaumbele cha kusajili beki mpya wa kati na mchezaji wa kimataifa wa Ecuador wa Bayer Leverkusen, Piero Hincapie mwenye umri wa miaka 22, yuko kwenye orodha yake. (***Bild***)

**GALLAGHER SAFARI IMEIVA**
KLABU ya Chelsea inaweza kutarajia kusajili wachezaji 11 msimu huu wa joto inapojaribu kupunguza kikosi chao kikubwa, huku kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 24, akiwa miongoni mwa wale wanaotarajiwa kuondoka.(***Sun***)

**PEDRI SAFI BARCA**
BARCELONA inajiandaa kumpa mkataba mpya kiungo wa kati wa Hispania, Pedri mwenye umri wa miaka 21, ambaye amekataa ofa ya Paris St-Germain. (***Fabrizio Romano***)

**GYOKERES KUIKAMUA ARSENAL**
MSHAMBULIAJI wa Sporting Lisbon na Sweden, Viktor Gyokeres analengwa zaidi na Arsenal, lakini mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 una kipengele cha kutolewa cha euro milioni 100.(***Football Transfers***)

**RABIOT SOKONI EPL**
KLABU ya Manchester United na Newcastle United imeripotiwa "kuanzisha mazungumzo" na kiungo wa kati wa Juventus na Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29, ambaye anaweza kupatikana kwa uhamisho wa bure msimu huu wa joto. (***Calciomercato***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KANE ASEMA HATAKI KUREJEA EPL HARAKA

### ●●● Nahodha huyo wa England ana matumaini ya kufanya vyema...

**MUNICH,** Ujerumani

HARRY Kane amesema 'anaangazia sana' maisha yake ya soka katika klabu ya Bayern Munich inayoshiriki Bundesliga, na inaonekana hatarejea haraka kwenye Ligi Kuu England.

**Kane alimaliza ushirika wa miaka 19 na Tottenham Hotspur msimu uliopita wa joto, na kuigharimu Bayern Munich euro milioni 100 pamoja na nyongeza ya euro milioni 10 na kufanya usajili ghali zaidi wa Ligi Kuu Ujerumani.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 amepata mafanikio makubwa katika maisha yake yote ya soka, akishinda tuzo tatu za Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England, Kiatu cha dhahabu cha Kombe la Dunia mwaka, 2018 pamoja na kuwa mfungaji bora wa muda wote wa England.

Lakini Kane hajawahi kunyanyua taji lolote katika ngazi ya klabu au kimataifa na ndio sababu kubwa iliyomfanya kuhamia Bayern Munich.

Katika hali isiyotarajiwa, Bayern wako mbioni kusalimisha taji lao la Bundesliga kwa Bayer Leverkusen, huku wakiambulia kipigo cha aibu cha Kombe la Ujerumani kutoka kwa timu ya Daraja la Kwanza, FC Saarbrucken mechi iliyochezwa Novemba, mwaka jana.

Lakini bado wana nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuwabana Arsenal kwa sare ya 2-2 katika mchezo wa kwanza wa robo fainali, mchezo ambao Kane alifunga kwa penalti.


Baada ya mchezo huo, nahodha huyo wa England aliulizwa kuhusu uwezekano wa kurejea Ligi Kuu England, ambapo alikataa.

"Ninafurahia sana uzoefu wangu nchini Ujerumani na ilikuwa hatua ambayo nilihitaji katika kazi yangu kwa ajili ya kichocheo kipya, changamoto mpya na mazingira mapya, viwanja vipya, timu mpya na nina furaha sana.

Ni kweli, najua jinsi Ligi ya England ilivyo kubwa, nilicheza huko kwa miaka mingi iliyopita na mustakabali wangu ni Bayern Munich. Nina mkataba wa miaka minne, ninaufurahia sana, natumani nitaweza kufanya kitu maalum msimu huu.

"Lakini kama sivyo, nitakuwa tayari kwenda tena msimu wa joto na kubadilisha mambo. Umekuwa msimu wa kukatisha tamaa katika Bundesliga hasa ukilinganisha na Bayer Leverkusen."

# VARANE PIGO JINGINE MANCHESTER UNITED




**MANCHESTER,** England

MLINZI wa kati wa Manchester United, Raphael Varane atakuwa nje ya uwanja kwa wiki kadhaa kutokana na jeraha la misuli huku Jonny Evans ataukosa mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Bournemouth utakaochezwa wikendi hii, klabu hiyo imetangaza.

Wachezaji hao walipata majeraha wakati United ilipopoteza 4-3 kwenye mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Chelsea wiki iliyopita, wakiungana na walinzi wengine, Lisandro Martínez na Victor Lindelof.

Mfaransa Varane mwenye umri wa miaka 30, anatumaini kurejea kabla ya mwisho wa msimu na Evans anatarajiwa kuwa nje ya dimba kwa muda mfupi, ilisema United katika taarifa yake.

Kikosi cha Kocha Erik ten Hag, ambacho kipo nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu England, kimekumbwa na majeruhi ya walinzi wakuu msimu huu.

Pamoja na Martínez na Lindelof, beki wa kushoto, Luke Shaw atakuwa nje ya uwanja kwa wiki chache zijazo, Harry Maguire na Aaron Wan-Bissaka wamekosa michezo mingi na huku beki wa kushoto Tyrell Malacia hajaonekana tangu alipofanyiwa upasuaji wa goti mwaka jana.

United wamebakiza mechi saba za kampeni na wanakabiliwa na vita ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

# Amorim: Bado Sijafikia makubaliano na Liverpool

**LISBON,** Ureno

KOCHA wa Sporting CP, Ruben Amorim, amecheka na kukana ripoti amefikia makubaliano ya kuwa kocha mpya wa Liverpool.

Iliripotiwa nchini Ujerumani mapema wiki hii makubaliano kati ya Amorim na Liverpool yalikuwa yamefikiwa, lakini mazungumzo na wakala wa kocha huyo mwenye umri wa miaka 39 hayajafikia hitimisho kama hilo.

Wakati wa mkutano wa waandishi wa habari, Amorim aliulizwa kama kulikuwa na ukweli wowote kwa uvumi huo ambapo alikataa.

"Ili kukomesha kila kitu, hii ndiyo mara yangu ya mwisho kuzungumzia mustakabali wangu," alisema.

„Kitu pekee ambacho sote tunataka hapa ni kuwa mabingwa na hakuna kitakachobadilisha hilo. Nitasema tena: Mimi ni Kocha wa Sporting. Hakukuwa na mahojiano na klabu yoyote, hakuna makubaliano na klabu yoyote."

90min inaelewa Liverpool imezungumza na wakala wa Amorim na suala la kifedha linaweza kujadiliwa, lakini vyanzo vimesisitiza hii ni kawaida katika hatua hii ya kutafuta mrithi wa Jurgen Klopp na hakuna uamuzi wa mwisho uliofikiwa.

Iwapo Liverpool watachagua kumwajiri Amorim, watahitaji kukubaliana ada ya fidia na Sporting.

Bosi huyo ana kipengele cha kuondoka cha euro milioni 20m kwa klabu isiyo ya Ureno, lakini Liverpool inaweza kujaribu kujadili punguzo.



# Inter Milan yamtaka Martial

**MILAN,** Italia

VINARA wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Inter Milan inaweza kuwasilisha ofa kwa Anthony Martial kabla ya kumalizika kwa mkataba wake Manchester United, kwa mujibu wa ripoti.

Sio mara ya kwanza kwa Martial kuhusishwa na kutaka kuhamia timu hiyo ya Italia, lakini sasa ripoti zinasema Inter ipo tayari kufikiria kumnunua tena mshambuliaji huyo wa Ufaransa.

Gazzetta dello Sport limeandika usajili wa Martial unajadiliwa na wakuu wa Inter, lakini wanashiriki wasiwasi juu ya kiwango chake duni na rekodi ya majeraha.

Martial haonekani kama kipaumbele chao katika ushambuliaji, ingawa mlengwa wao mkuu, Albert Gudmundsson wa Genoa, ambaye ana mkataba na klabu yake hadi 2027 na amekuwa akihusishwa na Tottenham katika miezi ya hivi karibuni.

Kuhama kwa Gudmundsson kutahitaji ada kubwa, na kwa hiyo ikiwa Inter itashindwa kumchukua mchezaji huyo wa kimataifa wa Iceland, nguvu zao zitahamia kwa Martial.

Faida ya kuhamia Martial kuliko Gudmundsson ni Inter haitalazimika kulipa ada ya uhamisho kwenda United, wakati hali yake kama mchezaji huru msimu huu wa joto inamaanisha wanaweza kuzungumza moja kwa moja kwenye kambi ya mchezaji huyo mara moja.

Kuhamia Serie A kunaweza kumfaa Martial, ambaye atakuwa anatazamia kuanza upya kujiimarisha kufuatia kampeni mbaya katika Ligi Kuu England.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 amecheza mara 19 katika mashindano yote msimu huu, akifunga mara mbili pekee.

Kinyume chake, Gudmundsson amezifumania nyavu mara 12 katika mechi 29 za Serie A.

Martial amefunga mara 90 katika mechi 317 akiwa na United tangu ajiunge nayo mwaka 2015 akitokea Monaco.



# MAFUNZO YAITOLEA MACHO 'TOP 4' LIGI KUU ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

TIMU ya Mafunzo imesema malengo yao msimu huu ni kuhakikisha wanamaliza katika nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha timu 16.

Kwa sasa Mafunzo ipo katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 29, Maafande hao wameshinda michezo saba, wametoka sare mechi nane na wamepokea vichpo katika michezo mitano.

Mafunzo imecheza mechi 20 za ligi hiyo ambayo ilisimama kupisha mwezi wa Ramadhani ambao umemalizika hivi karibuni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mafunzo, Abdallah Bakari "Edo" alisema kasi waliyoanza nayo katika michezo mitano kabla ya kusimama kwa ligi ndio watakayoendelea nayo baada ya ligi hiyo kurejea tena.

Edo alisema ameshapoteza matumaini ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar lakini wana nafasi ya kupambana na kuhakikisha wanamaliza nafasi nne za juu.

"Huku katika upande wa mbio za ubingwa kwa msimu huu kwetu ni vigumu kwa sababu hatukuwa na mwanzo mzuri wa katika ligi," alisema Edo.

**Aliongeza hata kama hawapo katika mbio za ubingwa lakini watajita hidi kufanya vizuri ka tika michezo yao 10 iliyobakia ili kuendeleza ushindani.**

„Tunataka kuonyesha ushindani katika mechi zilizosalia, tumejiandaa kucheza kwenye kiwango bora, kuwa na mwendelezo mzuri ndani ya ligi katika hatua hii ya lala salama.

Tumepanga kuwatumia wachezaji wetu wote ambao afya zao zimeimarika, nyota waliokuwa majeruhi wamepona, hii ni kwa mujibu wa daktari wa timu," Edo aliongeza.

Hata hivyo kocha huyo alisema ili kufanikisha mpango huo lazima timu yake ipate hamasa kutoka kwa mashabiki ili wachezaji wapambane katika kila mechi watakayocheza.



Wachezaji wa Yanga Princess wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumaliza mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania dhidi ya Baobab Queens itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Moro Kids yawaadhibu Bukombe

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Moro Kids imetinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Mikoa baada ya kuifunga Bukombe Combaine ya Geita mabao 5-2 katika mechi ya Kundi A iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

Wakati Moro Kids ikisonga mbele, Gunners ya Dodoma pia imekata tiketi ya kucheza hatua ya nusu fainali ya ligi hiyo baada ya kutoka suluhu dhidi ya Eagle ya Dar es Salaam.

Moro Kids na Eagles kwa sasa zinasubiri wapinzani kutoka Kundi B ili kucheza mechi za hatua ya nusu fainali na pamoja na kusaka bingwa na timu mbili zitakazopanda daraja kuelekea First League msimu ujao.

Kocha Mkuu wa Moro Kids, Ally Mbaruku, amesema haikuwa kazi rahisi kutinga hatua hiyo kwa sababu wapinzani wao walikuwa wazuri.

"Tulipotoka droo mechi iliyopita nilitoa ahadi mechi ya mwisho tutashinda, tumefanya hivyo ingawa mechi haikuwa rahisi, tunashukuru tumepata pointi tatu na mabao matano ambayo yametuwezesha kusonga mbele," alisema kocha huyo.

Mabao ya Moro Kids katika mechi hiyo yalifungwa na Amosi Saidi (mawili) na Saidi Hamisi ambaye amelifunga hat- trick huku yale ya Bukombe Combaine yote mawili yalipachikwa na Saido Ibrahim.

## *FIFA yaifungia Yanga kusajili*

INATOKA UK. 24

dogo madogo ambayo huwa anayaona na anayarekebisha.

"Tunatambua kila timu ipo katika mashindano hivyo imejiandaa vizuri, utakuwa mchezo mgumu lakini tunahitaji ushindi kuhakikisha tunatetea taji la Ligi Kuu Tanzania Bara," Gamondi alisema.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga inaongoza ikiwa na pointi 52 zilizovuna katika michezo 20 wakati Singida Fountain Gate iko nafasi ya saba, imejikusanyia pointi 24 baada ya kushuka dimbani mara 21.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA.

## Simba SC kibaruani ikiwataja mashabiki

INATOKA UK. 24

hatutawaangusha katika mchezo wetu huu, wasituache waje kutupa sapoti," alisema Matola.

Nahodha Msaidizi wa timu hiyo, Mohamed Hussein ,Zimbwe Jr' alisema wamejipanga kupambana zaidi na kuhakikisha wanashinda mechi hiyo ili kupunguza pengo la pointi kati yao na timu zilizoko juu yao kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Tunahitaji kushinda ili kuhakikisha haturuhusu pengo la pointi baina yetu na wanaoongoza, lakini haliwezi kufanyika kama mashabiki hawawezi kujitokeza kuja kutushangilia, sisi kama wachezaji tunawahitaji wao, tayari kuna vitu tumevizungumza wachezaji wenyewe ambavyo siwezi kuviongea hadharani, kurekebisha hapa na pale.

Kwa maana hiyo, tunawaahidi matokeo mazuri, kwa sababu mechi tatu za nyuma hatujafanya vizuri, tutapambana," alisema beki huyo wa kushoto.

Kocha wa Ihefu, Mecky Maxime, amesema pamoja na uzuri wa Simba, hata wao hawapo katika nafasi nzuri sana, hivyo wanazihitaji sana pointi tatu.

"Tunajua tuna mchezo mgumu dhidi ya Simba, kikubwa sisi kwenye Ligi Kuu bado hatuna matokeo ya kuridhisha, kwa hiyo pointi tatu tunazitaka. Mashabiki waje kwa wingi, mechi itakuwa nzuri kwa sababu Simba ni moja kati ya timu kongwe nchini, wana kikosi bora, ila bahati mbaya wametolewa katika mechi za kimataifa na wanajipanga tena ya kutaka kushiriki msimu ujao," Maxime alisema.

Simba iliyoshuka dimbani michezo 19 ipo katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 45 huku Ihefu ikiwa katika nafasi ya 11 na pointi zake 23 kibindoni lakini imecheza mechi 21.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Geita Gold dhidi ya Mtibwa Sugar huku JKT Tanzania itawafuata Tabora United na Kagera Sugar watakuwa wenyeji wa Dodoma Jiji FC kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba mkoani, Kagera.

# Michezo

Jumamosi Aprili 13, 2024

Nipashe




Kane asema hataki kurejea EPL haraka UK. 21



Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto (kushoto), akiwa na straika wa timu hiyo, Stephanie Aziz Ki, muda mfupi kabla ya kupanda ndege kurejea Dar es Salaam wakitokea Dodoma kuwavaa wenyeji Dodoma Jiji FC katika mechi ya michuano ya Kombe la FA. **PICHA: MTANDAO**

## Simba SC kibaruani ikiwataja mashabiki

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupoteza mechi tatu mfululizo, Simba itakuwa na na nafasi ya kujiuliza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu (sasa Singida Black Stars) itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Liti, mkoani Singida.

Simba itashuka dimbani na kumbukumbu ya kufungwa nyumbani na ugenini na Al Ahly ya Misri, katika mechi za robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku Jumanne iliyopita ikiondolewa kwenye mashindano ya Kombe la FA na Mashujaa FC ya Kigoma kwa kufungwa penalti 6-5 baada ya sare ya bao 1-1 kwenye dakika 90 za kawaida.

Wachezaji wa Simba, benchi la ufundi na viongozi wa timu hiyo wamewaangukia na kuwaomba mashabiki ‚wajazane' kwa wingi uwanjani ili kuishangilia na kamwe wasisuse.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, aliliambia gazeti hili mechi hiyo haitakuwa rahisi, lakini ameahidi kutowaangusha tena mashabiki kwa sababu wanajua wameumia kutokana na timu yao kutofanya vyema.

„Haitakuwa mechi rahisi, ni ngumu, Ihefu (Singida Black Stars), imesajili vizuri, ina kikosi kizuri, wamekuwa na matokeo mazuri katika mechi zao ilizocheza, sisi tunalielewa hilo, tumefanya maandalizi mazuri, tutahakikisha ni lazima tupate matokeo mazuri katika mechi hii.

Kikubwa niwape pole matokeo yaliyopita, hakuna asiyejua mmeumia katika mechi iliyopita, lakini tuna hakika

INAENDELEA UK. 23

# FIFA yaifungia Yanga kusajili

## TFF pia yapigilia 'nyundo', Gamondi afurahia viwango...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI ikijipanga kuhakikisha inashinda kila mechi watakayocheza, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga imefungiwa kufanya usajili wa wachezaji kwa sababu imekiuka kanuni za Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu (FIFA), imefahamika.

Hata hivyo FIFA na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), hazikutaka kuweka wazi jina la mchezaji ambaye usajili wake umesababisha Yanga kukumbana na adhabu hiyo.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema jana uamuzi wa kuifungia Yanga umefikiwa baada ya klabu hiyo ya Mitaa ya Jangwani na Twiga, Dar es Salaam kukiuka "Annex 3 " ya Kanuni ya Uhamisho wa mchezaji (RSTP) ya FIFA.

**Ndimbo alisema pamoja na masuala mengine Yanga haikuingiza uthibitisho wa malipo ya uhamisho wa mchezaji husika katika mfumo wa usajili (TMS) licha ya kukumbushwa kufanya hivyo.**

"Klabu hiyo imetakiwa kutekeleza matakwa hayo ya kikanuni na kuwasilisha taarifa kwa sekretarieti ya Kamati ya Nidhamu ya FIFA ambapo suala hilo limefikishwa kwa ajili ya kuchukuliwa hatua zaidi.

Kutokana na uamuzi huo wa FIFA, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), pia imeifungia klabu hiyo kufanya usajili kwa wachezaji wa ndani ," alisema Ndimbo.

Lakini pia TFF haijafafanua adhabu ya kufungiwa Yanga itakuwa ya muda gani, kama usajili wa dirisha kubwa pekee, au mpaka pale itakapotimiza yaliyoagizwa na FIFA hata kabla ya dirisha la usajili kukamilika.

Nipashe ilipowasiliana na Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, kupata ufafanuzi kuhusiana na adhabu hiyo, kiongozi huyo hakupatikana.

Kuelekea mechi dhidi ya Singida Fountain Gate itakayochezwa kesho, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amewasifu wachezaji wake wanavyopambana mazoezini ili kuhakikisha wanakuwa imara na tayari kupata ushindi katika michezo yao iliyoko mbele.

Gamondi alisema hata katika michezo ambayo hawakupata ushindi, nyota wake hupambana na kinachowazuia ni suala la bahati.

"Ukiangalia wachezaji wanavyocheza unaona kabisa wanavyojitoa kwa ajili ya timu yao, tunapokosa ushindi tunakuwa tumekosa bahati tu lakini wachezaji wanakuwa wamefanya kazi yao kwa uhakika," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema kila wanapokuwa kwenye uwanja wa mazoezi wanatumia muda mwingi kusisitiza kuhusu hali ya upambanaji ili kupata matokeo mazuri kwa ajili ya kutimiza malengo.

Aliongeza asilimia kubwa anaridhishwa na viwango vya nyota wake ukiacha makosa ma-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >